**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# RIPOTI YA JUMLA YA UKAGUZI WA UFANISI NA UKAGUZI MAALUMU KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 MACHI, 2016

**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**Machi 2016**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

**Dira**
**Kuwa kituo cha ufanisi katika ukaguzi wa hesabu za Serikali na taasisi za Umma.**

**Dhamiri**
**Kutoa huduma za ukaguzi wa hesabu zenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.**
**Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:**

**Uadilifu**
**Kuwa taasisi adilifu inayotoa huduma bila upendeleo.**

**Weledi**
**Tunalenga kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu kwa kuzingatia taratibu bora.**

**Uaminifu**
**Tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa sheria.**

**Mkazo kwa watu**
**Tunalenga kufanikisha matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia wateja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.**

**Uvumbuzi**
**Kuwa taasisi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya taasisi.**

**Matumizi bora ya rasilimali**
**Kuwa taasisi inayothamini na kutumia kwa umakini mkubwa rasilimali za umma ilizokabidhiwa.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mtaa wa Samora , S.L. P 9080, Dar es Salaam
Simu ya Upepo : “Ukaguzi", Simu: 255(022)2115157/8, Nukushi: 255(022)2117527, Barua Pepe: **ocag@nao.go.tz**,
Tovuti : **www.nao.go.tz**

Kwa majibu tafadhali taja Kumbukumbu:
**Na. FA 27/249/01/2014/2015**

**28 Machi, 2016**

Mheshimiwa Dkt. John P. Magufuli,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
Barabara ya Barack Obama Na 1
**11400 Dar es salaam.**

**Yah: KUWASILISHA RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZA RIPOTI SITA ZA UKAGUZI WA UFANISI**

Kwa mujibu wa ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa mwaka 2005) na kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha kwako ripoti yangu ya saba ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu.

Taarifa hii inajumuisha taarifa sita za Ukaguzi wa Ufanisi ambazo zinahusu Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zitakazowasilishwa Bungeni mnamo mwezi Aprili 2016.

Nawasilisha.

Prof. Mussa Juma Assad
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

# YALIYOMO


**ORODHA YA VIFUPISHO ........ X**

**DIBAJI........ XI**

**SHUKRANI ........ XIV**

**MUHTASARI KWA WAANDAMIZI........ XVI**

**SURA YA KWANZA........ 1**

**UTANGULIZI ........ 1**

1.1 Usuli wa Ukaguzi ........ 1
1.2 Mamlaka ya Kukagua ........ 1
1.3 Madhumuni ya Ripoti ........ 2
1.4 Lengo Kuu la Ripoti ........ 3
1.5 Mchakato wa Uthibitisho wa Takwimu ........ 3
1.6 Muundo wa Ripoti ........ 3

**SURA YA PILI ........ 5**

**USIMAMIZI WA UTENDAJI KATIKA TAASISI ZA UMMA........ 5**

2.1 Utangulizi........ 5
2.2 Usimamizi wa Data ........ 5
2.3 Upimaji wa Utendaji kwenye taasisi za umma ........ 7
2.4 Ufuatiliaji wa utekelezaji katika tasisi za umma ........ 8
2.5 Uhusiano kati ya usimamizi wa taarifa, upimaji wa utekelezaji, na ufuatiliaji wa utekelezaji 10

**SURA YA TATU........ 11**

**USIMAMIZI WA DATA KWENYE SEKTA YA UMMA ........ 11**

3.1 Utangulizi........ 11
3.2 Malengo ya usimamizi wa data kwenye sekta ya umma ........ 11
3.3 Uandaaji na uzalishaji wa data ........ 12
*3.3.1 Mapungufu katika upatikanaji wa data ........ 12*
*3.3.2 Udhaifu katika uzalishaji na uhakiki wa data........ 13*
*3.3.3 Mapungufu ya data kwa ajili ya kufanya maamuzi........ 17*
3.4 Uhifadhi wa kumbukumbu ........ 18
*3.4.1 Ukosefu wa mifumo ya kukusanya na kuhifadhia data (data za awali)18*
*3.4.2 Udhaifu katika mifumo ya kurekodi data ........ 20*
3.5. Usahihi wa Data........ 21
3.6 Matumizi na Uwasilishaji wa Data........ 23

*3.6.1 Mapungufu katika matumizi ya data wakati wa kuandaaa mipango kazi 23*
*3.6.2 Udhaifu katika kuwasilisha na kushirikishana data ....................24*
*3.6.3 Mrejesho kuhusiana na taarifa zilizowasilishwa ....................28*

**SURA YA NNE ....................31**

**UPIMAJI WA UTENDAJI ....................31**

4.1 UTANGULIZI ....................31
4.2 LENGO LA KUPIMA UTENDAJI KATIKA SEKTA YA UMMA ....................31
4.3 KUKOSEKANA KWA TATHMINI YA MATOKEO YA UTENDAJI KWA KUZINGATIA MALENGO ....................32
4.4 MKAZO FINYU KWENYE VIASHARIA VYA UTENDAJI AMBAVYO SI VYA UPIMAJI WA FEDHA ....................35
4.5 HAKUNA UHUSIANO KATI YA VIASHIRIA VYA UFANISI/ UTENDAJI NA MALENGO YA JUU YA TAASISI....42
4.6 KUTOKUANDAA MIPANGO YA UPIMAJI WA UTENDAJI ....................45

**SURA YA TANO ....................48**

**UFUATILIAJI KATIKA SEKTA YA UMMA ....................48**

5.1 UTANGULIZI ....................48
5.2 LENGO LA KUCHUNGUZA UFUATILIAJI KATIKA SEKTA YA UMMA ....................48
5.3 UFUATILIAJI KWENYE UTENDAJI WA SEKTA YA UMMA ....................49
5.4 TATHMINI KATIKA UTENDAJI WA SEKTA YA UMMA ....................55
5.6 MAWASILIANO KATIKA UTENDAJI WA SEKTA YA UMMA ....................59

**SURA YA SITA ....................66**

**HITIMISHO ....................66**

6.0 UTANGULIZI ....................66
6.1 USIMAMIZI WA DATA KWENYE SHUGHULI ZA SEKTA ZA UMMA ....................66
6.2 UPIMAJI WA UTENDAJI KWA TAASISI ZA SERIKALI ....................67
*6.2.1 Kushindwa kusimamia upimaji wa utendaji kwenye taasisi za serikali68*
6.3 UFUATILIAJI KATIKA SHUGHULI ZA SEKTA YA UMMA ....................69

**SURA YA SABA ....................71**

**MAPENDEKEZO ....................71**

7.1 UTANGULIZI ....................71
7.2 USIMAMIZI WA DATA KWENYE SHUGHULI ZA SEKTA YA UMMA ....................71
7.3 UPIMAJI WA KIUTENDAJI KWENYE TAASISI ZA UMMA ....................72
7.4 USIMAMIZI WA UFUATILIAJI KATIKA SEKTA YA UMMA ....................73

**MAREJEO ....................74**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| TAMISEMI | - | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TZS | - | Shilingi ya Tanzania |

# DIBAJI

Nina furaha kuwasilisha Ripoti yangu ya Saba ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu. Ripoti hii ya jumla inahusu taarifa saba za ukaguzi wa Ufanisi kwa serikali kuu (Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi; Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Fedha na Mipango; na Ofisi ya Makamu wa Raisi na Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa).

Ripoti hii inalenga kutoa taarifa kwa wadau (wabunge, maofisa wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, wanahabari, wafadhili, na asasi za kijamii na zisizo za kiserikali kuhusiana na matokeo ya ukaguzi yaliyopo kwenye ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu zilizofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kufikia Mwezi Machi 2016. Ufafanuzi wa kina kuhusiana na taarifa zilizoandikwa kwa kifupi unapatikana kwenye ripoti husika ya ukaguzi ambayo ilikabidhiwa kwa Maofisa Masuuli (Makatibu Wakuu) wa wizara husika.

Ripoti hii imekabidhiwa kwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa mujibu wa ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Vifungu 34 (1) na (2) vya sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya mwaka 2008.

Chini ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama inavyorekebishwa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila taarifa aliyotoa kwa mujibu wa Ibara ndogo (2) ya Ibara iliyotajwa. Mara taarifa hiyo inapopokelewa, Rais atamwelekeza waziri husika kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya kikao cha kwanza cha Bunge kabla ya siku saba kupita toka kikao cha kwanza cha Bunge kuanza. Ibara hiyohiyo inamruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha ripoti yake kwa Spika wa Bunge iwapo Rais kwa sababu zozote zile atashindwa kuwasilisha ripoti hiyo kwa Spika kama sheria inavyotaka.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008 kumeimarisha uhuru wa utendaji wa ofisi yangu katika kutimiza majukumu yake ya kikatiba. Uhuru wa utendaji wa ofisi yangu unatarajiwa kuniwezesha kupata na kuwa na udhibiti muhimu juu ya rasilimali zote zilizopo kwa ajili ya ofisi ikiwa ni pamoja na rasilimali watu na fedha, ambazo zitaiwezesha ofisi yangu kufanya kazi bila kuingiliwa na mtu au mamlaka yoyote ikiwemo zile ninazozikagua.

Sheria hii imepanua mawanda ya ukaguzi kwa kunipa mamlaka ya kufanya ukaguzi wa Ufanisi, wa Utambuzi, wa Mazingira na Maalumu.Aina hizi za ukaguzi ni zaidi ya ukaguzi wa kawaida wa Taarifa za Fedha kama ambavyo tumekuwa tukifanya kwa miaka mingi.

Kimsingi, taarifa hii imeniwezesha kutoa maoni huru kwa Bunge kuhusiana na matumizi sahihi na uwajibikaji, uwazi, na uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma kwenye maeneo ya Usimamizi wa Ubora wa Elimu, Uzalishaji nyama, Huduma za ugani, milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea,tathmini ya athari ya mazingira, na mikataba.

Lengo kuu la kufanya aina hizi za ukaguzi ni kuangalia kama rasilimali zilizotengwa zimetumika kwa ufanisi kwa kuzingatia uwekevu, tija, na ufanisi kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge kwenye maeneo yaliyotajwa.

Ni vizuri kufahamu kwamba wakati Ofisi yangu inafanya ukaguzi na kutoa taarifa ya utendaji wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, na Mashirika ya Umma kulingana na sheria katika taratibu zilizopo, wajibu wa kuhakikisha uwepo wa ufanisi, uwekevu, na tija katika matumizi ya rasilimali za umma ni wa Maofisa Masuuli. Wakati huohuo ni wajibu wa Maofisa masuuli kuhakikisha uchunguzi na mapendekezo niliyoyatoa yanatekelezwa kikamilifu.

Ni matarajio ya Bunge kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ataandaa taarifa za fedha kuhusu usimamizi wa rasilimali za umma katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma kuhusiana na tija na ufanisi kwenye utekelezaji wa programu mbalimbali za Serikali. Ofisi yangu inachangia kwa kutoa mapendekezo ili kuboresha utendaji katika sekta ya umma. Kwa jinsi hiyo, Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Ofisi yangu kwa pamoja zina mchango mkubwa kwa Bunge katika kujenga imani kwa Umma katika usimamizi wa rasilimali za umma. Ingawa majukumu yanatofautiana, matarajio ya usimamizi bora kwa rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya wabunge na umma kwa ujumla, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya mapitio ya njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta ya Umma. Aidha, tunahakikisha ukaguzi wetu unalenga na kuyapa kipaumbele maeneo muhimu yanayochangia maendeleo ya sekta ya umma. Hivyo kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa rasilimali za umma.

Ninapenda kutambua weledi na dhamira ya wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa juhudi kubwa walizofanya katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi, na mishahara duni na wakati mwingine kufanya kazi kwenye maeneo yasiyofikika kirahisi.

Ninatarajia kuwa Bunge, vyombo vya habari na jamii kwa ujumla itaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kutokana na jukumu lake la usimamizi wa rasilimali za umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania. Hivyo, nitafurahi kupata mapendekezo ya jinsi ya kuboresha taarifa kama hii kwa siku zijazo.

**Prof. Mussa Juma Assad,**
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,**

---

**Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,**
**Dar es Salaam.**
**29 Machi, 2016**

## SHUKRANI


Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioweka mazingira wezeshi kwangu kuweza kutimiza wajibu wangu wa kikatiba. Ninapenda kumshukuru kila mfanyakazi katika Ofisi yangu kwa jitihada zao ambazo zimeniwezesha kutoa ripoti kwa wakati. Ninalazimika kuishukuru familia yangu na za wafanyakazi katika Ofisi yangu kwa uvumilivu wao waliouonyesha wakati wa kipindi chote cha kutimiza wajibu huu wa kikatiba.

Ninapenda kuishukuru Serikali na Bunge letu tukufu kwa kuendelea kuisaidia Ofisi yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Vilevile, shukrani za pekee ziende kwa jumuiya ya wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden, Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden, Serikali ya Ujerumani kupitia GIZ, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani, Benki ya Dunia kupitia mradi wa "Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha" na wote waliotutakia mema ambao walichangia kwa njia moja au nyingine kwa nia ya kuleta mabadiliko katika Ofisi yangu. Mchango wao katika kuendeleza uwezo wa wafanyakazi kiujuzi, kimfumo wa teknolojia ya mawasiliano, na nyenzo mbalimbali vimechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio yetu.

Halikadhalika, ninapenda kuwashukuru wadau wengine wote ikiwa ni pamoja na maofisa Masuuli wa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi; Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Fedha na Mipango; Ofisi ya Makamu wa Rais; na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Vilevile ninapenda kuwasilisha taarifa za ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa miaka ya nyuma kwenye ripoti tano za ukaguzi wa ufanisi ambazo zilihusisha Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa ushirikiano walioutoa na kutupatia taarifa muhimu zilizohitajika wakati wa uandaaji wa ripoti za ukaguzi ambazo ni chanzo cha ripoti hii ya ujumla.

Shukrani za kipekee ziende kwa jamii ya wanataaluma na wataalamu wa kada mbalimbali kutoka Chuo Kikuu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, wataalamu wa kujitegemea, na maofisa wastaafu wa serikali kwa michango yao ambayo iliboresha ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi kupitia maoni na uhakiki walioufanya katika rasimu za ripoti hizo. Ninapenda pia kuishukuru Kamati ya Bunge Hesabu za Serikali Kuu ambayo ripoti hii pamoja na ripoti binafsi zitafikishwa kwa ajili ya uchunguzi, majadiliano, na kutoa maelezo yake. Tunatarajia kuwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu itatupa maboresho na muelekeo utakaotokana na mjadala wa ripoti hizi.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru Maofisa Masuuli na watumishi wote wa umma Tanzania nzima. Ninatambua pia mchango wa walipakodi ambao ripoti hii tunaitoa kwao. Mwenyezi Mungu awabariki wote kama mnavyojitoa katika kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma nchini.

## MUHTASARI KWA WAANDAMIZI

Ukaguzi wa Ufanisi unalenga kuboresha uwajibikaji na ufanisi wa taasisi za Umma. Pia unatoa tathmini ya haki na elekevu kuhusiana na namna taasisi zilizokaguliwa zinavyotumia rasilimali katika kutimiza majukumu yao kwa kuzingatia uwekevu, tija, na ufanisi. Kifungu namba 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya mwaka 2008 inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi wa Ufanisi.

Ripoti hii ya jumla inaainisha mapungufu yaliyobainika, hitimisho, na mapendekezo kwa ripoti zote sita za ukaguzi zilizofanyika kwa mwaka 2015 zinazohusiana na Mfumo wa Usimamizi wa Ubora wa Elimu Tanzania; Usimamizi wa Mikataba ya Ujenzi wa Miradi ya Maji Mijini; Usimamizi wa Mchakato wa Tathmini ya Athari za Kimazingira katika Miradi ya Maendeleo; Utekelezaji wa Mipango ya Usimamizi wa Milipuko ya Magonjwa na Wadudu waharibifu wa Mimea; Usimamizi wa Usafi katika Uzalishaji wa Nyama; na Huduma za Ugani. Mkazo umewekwa katika maeneo ya Usimamizi wa Taarifa, Upimaji wa Utendaji, na Ufuatiliaji katika Sekta ya Umma.

Kwa ujumla, ripoti hii ina lengo la kuwasaidia wabunge, serikali, vyombo vya habari, umma na wadau wengine kufanya maamuzi ili kuongeza uwekevu, tija, na ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za serikali. Hata hivyo, ripoti hii ya majumuisho hailengi kuwa mbadala wa ripoti sita ambazo zimefanyika na kuwasilishwa karibuni. Kwa mantiki hii basi msomaji anashauriwa kusoma ripoti za Ukaguzi husika ili kuweza kupata undani wa kilichokaguliwa.

Ripoti hii inatoa ufahamu kutokana na ripoti binafsi za Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu kiwango cha vyombo vya serikali katika usimamizi wa data, kupima utendaji wao, na kuendesha ufuatiliaji wa shughuli zao.

Yafuatayo yalikuwa matokeo muhimu ya uchunguzi uliofanywa:

### *Usimamizi wa data katika sekta ya umma*

Ukaguzi ulibaini udhaifu katika namna taasisi za serikali zinavyosimamia data. Taasisi hazikuhifadhi, hazikuzalisha, hazikudumisha, hazikutumia na hazikuwasilisha data katika utendaji wa shughuli zao. Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Usafi katika Uzalishaji wa Nyama ulibainisha kuwa mifumo ya data ya Mamlaka ya Chakula na Dawa, Wizara ya Afya, Wizara ya Mifugo, na TAMISEMI haikufanya kazi kwa ufanisi. Wizara ya Afya haikufuatilia kikamilifu shughuli za Mamlaka ya Chakula na Dawa

Taarifa hazikuzingatia usafi wa nyama na hakuna data zilizokuwa zinapatikana katika TAMISEMI zinazoonyesha utendaji wa Idara ya Mifugo licha ya kuwa na mratibu anayehusika na sekta hiyo. Wizara ya Mifugo na Mamlaka ya Chakula na Dawa hazikuandaa na kuzalisha data muhimu kuhusiana na idadi ya machinjio yaliyosajiliwa. Katika ukaguzi wa Usimamizi wa Ubora wa Elimu ilionekana kwamba Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais-TAMISEMI hazikuweza kutoa takwimu kuhusu utendaji wa vituo vya kujengea uwezo walimu. Kulikuwa na matukio ambapo taasisi zilizokaguliwa zilishindwa kuthibitisha taarifa zilizotumika kuandaa nyaraka muhimu. Vilevile, Ukaguzi wa Usimamizi wa Mikataba ya Ujenzi wa Miradi ya Maji Mijini ilikuwa na udhaifu katika kuhakiki data zilizotumika kuandaa makadirio ya gharama za ujenzi (Makadirio ya Ujenzi). Hali hii ilisababisha ongezeko la gharama za ziada kutokana na kurekebisha makosa yaliyofanywa.

Ukaguzi ulibainisha udhaifu katika kuweka na kutunza kumbukumbu za taasisi husika. Kwa mfano, ukaguzi wa Usimamizi wa Machinjio uligundua kuwa machinjio matano (5) kati ya kumi na mbili (12) yaliyotembelewa hayakuwa na kumbukumbu za taarifa za uchunguzi wa awali wa magonjwa ya wanyama kabla hawajachinjwa.

Kulikuwa pia na udhaifu katika mawasiliano na kubadilishana taarifa kati ya taasisi za serikali. Kwa mfano, katika ukaguzi wa Usimamizi wa Machinjio, ilibainika kwamba Mamlaka ya Chakula na Dawa na Serikali za Mitaa hazikuwa zinawasilisha ripoti zao za ukaguzi kwa wadau muhimu ambao wanatakiwa kupokea ripoti hizo. Serikali za Mitaa mara chache ziliwasilisha matokeo ya ukaguzi kwa tawala za mikoa na TAMISEMI lakini hazijawahi kupeleka taarifa hizo wizarani (Wizara ya Mifugo na Wizara ya Afya). Matokeo yake, mapendekezo ambayo walipewa kutokana na ukaguzi uliofanyika hayakufanyiwa kazi vya kutosha na Serikali za Mitaa. Kadhalika, ukaguzi wa Usimamizi wa Mikataba umebaini kuwa Wizara ya Maji haikufanya maamuzi ya kuwasiliana na wataalamu washauri na wakandarasi. Katika baadhi ya matukio, mawasiliano haya yalitolewa kwa mdomo bila ya kumbukumbu za maandishi.

### *Upimaji wa Utendaji katika Sekta ya Umma*

Tasisi zilizokaguliwa zilikosa mifumo ya kupima utendaji wa taasisi zao na ule wa taasisi zilizo chini ya mamlaka yao. Hii ilisababishwa na mambo mawili: Kwanza, kwa kiasi kikubwa upimaji wa utendaji katika sekta ya umma umelenga kungalia utendaji wa kifedha zaidi kwa kulinganisha kiasi cha fedha kilichotengwa na matumizi yake badala ya kuzingatia mapungufu katika utoaji wa huduma. Pili, sekta ya umma haioni umuhimu wa upimaji wa utendaji katika utoaji wa huduma kwakuwa hufanyika tu wakati wa kazi zenye ufadhili.

Utambuzi na uchaguzi wa viashiria vya utendaji kwa ajili ya kupima utendaji wa taasisi za sekta ya umma katika utoaji wa huduma zao au utekelezaji wa miradi ya maendeleo haufanyiki vya kutosha. Ilibainika kuwa taasisi tisa zilizokaguliwa zimeshindwa kuanzisha malengo ya upimaji wa utendaji wa huduma zao zinazotolewa kwa watu. Matokeo yake, taasisi zilitoa tu taarifa juu ya utendaji wa kifedha huku zikipuuza masuala yanayohusiana na ubora na muda wa kuhudumia watu. Kwa mfano, katika Ukaguzi wa Usimamizi wa Mikataba ya Ujenzi, ukosefu wa kipimo cha utendaji ulisababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi ya maji kwa kipindi cha kati ya miezi tisa na miaka minne. Hali hii ilisababisha ongezeko la gharama za mradi zilizofikia hadi shilingi bilioni 3.7.

Pia kulikuwa na udhaifu katika kuchukua hatua za maboresho na udhaifu katika utoaji mrejesho. Hali hii ilisababishwa na mawasiliano duni ya kiutendaji miongoni mwa wadau muhimu ambapo kulikuwa na mawasiliano ya upande mmoja kutoka chini kwenda juu. Pia, hakuna mrejesho uliotolewa kwenda Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa na Wizara husika kuhusiana na taarifa iliyowasilishwa kwao. Taarifa nyingi kutoka TAMISEMI, Wizara husika na Tawala za Mikoa zilikuwa ni za maelekezo na zilitolewa kwa nadra sana. Tawala za Mikoa zilizikumbusha Serikali za Mitaa kuzipelekea data hasa pale walipoacha kupeleka ripoti za utekelezaji za kila mwaka kwa tawala za mikoa. Aidha, ilibainika kuwa hakuna taasisi kati ya zilizokaguliwa iliyoweza kutafsiri ripoti zao ili kuonesha mwenendo wa utoaji wa huduma katika maeneo yao.

### *Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa shughuli **katika** Sekta ya Umma*

Ukaguzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Ubora wa Elimu umebaini udhaifu unaotokana na ufuatiliaji hafifu. Kwa mfano, kukosekana kwa mpango wa maendeleo ya walimu kitaaluma ilikuwa moja ya sababu za kuwepo walimu wasiokuwa na sifa. Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa vyombo vya kufuatilia maendeleo ya waalimu kitaaluma. Kukosekana kwa mpango sahihi wa mafunzo kwa walimu walioko kazini kulisababishwa na Wizara ya Elimu kukosa chombo cha kufuatilia utekelezaji wa shughuli za mafunzo. Ukosefu wa orodha ya vitabu teule vya kutumika katika kufundishia na kujifunzia kunaashiria udhaifu katika ufuatiliaji wa vitabu. Hii pia ilisababisha uwepo wa vitabu vingi katika soko ambavyo havijahakikiwa ubora wake. Hata hivyo, matokeo ya ukaguzi wa shule hayakushughulikia tatizo hili.

Ukaguzi wa usafi katika mchakato wa uzalishaji nyama pia umebaini udhaifu katika ufuatiliaji ambao ulisababisha kukithiri kwa tabia za uchafu katika mchakato wa uzalishaji nyama. Shughuli za kuchinja zilifanywa katika mazingira yasiyofaa kwa afya za walaji kutokana na udhaifu wa utaratibu wa ufuatiliaji wa usafi katika machinjio. Udhaifu katika utaratibu wa ufuatiliaji ulionekana katika ngazi mbalimbali za taasisi za umma. Hii ilisababishwa na uwepo wa machinjio ambayo hayajasajiliwa.

Uchunguzi wa kubaini uwepo wa magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao haukufanyika kama ilivyotakiwa kwa sababu mfumo wa ufuatiliaji haukushughulikia eneo hili. Ufuatiliaji hafifu ulipelekea kukosekana kwa mipango inayozingatia vihatarishi kwa ajili ya usimamizi wa milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao.

Ukaguzi umebaini udhaifu wa namna ambayo taasisi zinavyosimamia tathmini ya utendaji. Ilibainika kuwa taasisi za serikali hazijitathmini vya kutosha katika utendaji wao hasa katika shughuli wanazofanya. Kwa mfano, kuwepo kwa walimu wasiokuwa na sifa kama ilivyoripotiwa katika Ukaguzi wa Mfumo wa Kusimamia Ubora wa Elimu,ulionekana ni ishara ya udhaifu katika idara zinazohusika na utoaji wa elimu kujitathmini binafsi. Iwapo kungekuwepo na kujitathmini kungesaidia kutambuliwa na kuondolewa kwa tatizo la uwepo wa walimu wasiokuwa na sifa.

Mawasiliano hafifu ya matokeo ya usimamizi yalionekana katika kaguzi 4 kati ya 6 zilizofanyika kwenye taasisi za serikali. Kujirudia kwa udhaifu katika sekta ya umma inaweza kuwa imesababishwa na mikakati duni ya mawasiliano. Kwa ujumla, udhaifu ulioonekana ulihusu kukosekana kwa malengo ya mawasiliano ili kuwezesha kufahamu: nini cha kuwasiliana na kwa nani; namna ya kuwasiliana; muda wa kuwasiliana; na kutathmini kinachotarajiwa katika mawasiliano hayo. Ukaguzi wa mfumo wa kudhibiti ubora wa elimu umebaini mapungufu katika mawasiliano. Matokeo ya mitihani yalikuwa chombo cha kutathmini utendaji na kubaini mapungufu ili kuboresha ubora wa elimu. Matokeo ya mitihani yalilenga kuwapa wadau taarifa zinazohitajika kwa ajili ya maboresho. Hata hivyo, ilibainika kuwa matokeo ya mitihani hayakutumika kuboresha taasisi zinazohusika katika utoaji wa elimu.

Taarifa za uchambuzi wa matokeo ya mitihani hazikutolewa na wala kusambazwa kwa wakati. Hivyo, taasisi zinazohusika na zinazoshiriki katika utoaji wa elimu nchini hazikutumia taarifa hizo kwa ufanisi kuweka mipango ya kuzingatiwa kwa ajili ya utendaji wa taasisi. Kwa upande mwingine, mawasiliano hafifu au yanayocheleweshwa yanaweza kusababisha utekelezaji duni wa mapendekezo yaliyotolewa. Hii ni kama inavyothibitishwa katika ripoti ya Ukaguzi wa Usafi katika uzalishaji wa nyama ambayo taarifa duni ya utekelezaji wa mapendekezo ilionekana. Moja ya mapendekezo yaliyotolewa na Mamlaka ya Chakula na Dawa kwa Halmashauri kutokana na ukaguzi na ufuatiliaji wa ripoti yalionyesha mambo ambayo ni lazima kushughulikiwa kutokana na kasoro ndogo katika uendeshaji na katika kuboresha mazingira. Mambo hayo ni pamoja na kuondoa sakafu iliyochakaa, kuboresha mfumo wa usimamizi wa taka, kuhakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha, na utupaji sahihi wa taka. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi kwamba mapendekezo hayo yaliwasilishwa kwenye Serikali za Mitaa husika kwa hatua za marekebisho.

## HITIMISHO

### Usimamizi wa data katika sekta ya umma

Taasisi za serikali hazizalishi na kuhifadhi katika kiwango cha kutosha data zinazopatikana katika vyanzo mbalimbali. Kuna udhaifu katika mapitio ya data zinazopatikana ndani na nje ya taasisi. Matokeo yake data potofu zinatumika bila kuzirekebisha. Hii ni kutokana na ukosefu wa utaratibu wa wazi wa kuwezesha kuhakiki data zinazozalishwa. Mfumo wa kuhifadhi data ni dhaifu (utunzaji kumbukumbu). Taasisi za serikali hazihifadhi vya kutosha kumbukumbu za shughuli ambazo zinazitekeleza. Data zinazopatikana katika taasisi ni hafifu kuwezesha taasisi au mtumiaji wa data hizo kufanya maamuzi.

### Upimaji wa utendaji katika sekta ya umma

Upimaji wa utendaji katika taasisi za sekta ya umma haukufanywa vizuri na hivyo kuna udhaifu katika kupima na kuelewa kiwango cha utendaji wa vyombo mbalimbali vya sekta ya umma. Hii ni kwa sababu vyombo vingi vya serikali havina mifumo mizuri ya upimaji wa maendeleo ya utendaji inayoweza kutumika kuongoza na kuelekeza kila taasisi za umma namna ya kutathmini utendaji wake katika kutoa huduma kwa watu.

## Ufuatiliaji katika sekta ya umma

Kuna udhaifu katika usimamizi, tathmini, na mawasiliano katika taasisi zilizokaguliwa. Hii imeathiri utendaji mzima wa shughuli na utoaji wa huduma kwa umma. Wadau hawatekelezi kwa ufanisi majukumu yao kwa sababu hawapati taarifa kwa wakati muafaka. Uratibu mzuri kati ya wadau unahitaji uwepo wa mawasiliano sahihi na kwa wakati katika hatua za awali za uanzishaji na ushiriki katika utekelezaji hadi hatua ya mwisho ya mradi. Ni vigumu sana kutathmini shughuli ambayo haikuandaliwa vizuri na ambayo maendeleo yake hayasimamiwi kwa utaratibu na matokeo ya taarifa kuwasilishwa.

Kadhalika, tathmini haifanyiki katika kiwango cha kutosha. Mapungufu katika ufuatiliaji, tathmini, na mawasiliano ya matokeo ya utendaji yanazuia upatikanaji wa taarifa sahihi ambazo zingeweza kutumika kwa ajili ya maboresho ya siku zijazo.

## MAPENDEKEZO

Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kuwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika, Wakala na Malamlaka za Serikali za Mitaa zote:
*Usimamizi wa data:*

i Zinaanzisha na kuboresha mifumo ambayo itawawezesha upatikanaji na utunzaji sahihi wa data zinazopatikana kutoka katika vyanzo mbalimbali kwa matumizi ya kiofisi na utekelezaji wa shughuli zilizoainishwa;

ii Zinaanzisha mfumo wa mapitio ili kuhakikisha kuwa data zote zinazopokelewa kutoka vyanzo mbalimbali zinahakikiwa ili kuhakikisha kuwa ni kamili na sahihi kabla ya kutumika;

iii Kuendeleza mifumo ya wazi kwa ajili ya kudumisha data ili kuwezesha uwepo na upatikanaji wa taarifa kwa watumiaji walengwa;

iv Zinaanzisha mbinu na mikakati ya wazi ya usimamizi wa data ili kushughulikia masuala ya ubora wa data katika sekta ya umma;

v Zinaanzisha mfumo wa wazi unaoeleweka wa kubadilishana data kwenye sekta ya umma wakati zitakapohitaji; na

vi Kutoa mrejesho kulingana na ripoti zinazowasilishwa kwa ajili ya maboresho au maamuzi muhimu.

*Upimaji wa utendaji:*

vii Kupitisha na kutumia upimaji wa utendaji na kwa njia hiyo taarifa za utendaji za mwaka za kila taasisi zizalishwe na kutumika kama kipimo cha kutathmini kiwango chao cha utendaji katika utoaji wa huduma;

viii Kuanzisha mfumo wa utendaji kwa ajili ya huduma zote zilizotolewa; na kutoa hadhi ya utekelezaji kwa kufanya tathmini ya mara kwa mara juu ya utendaji wao;

ix Kuwepo na utambuzi na uchaguzi sahihi wa viashiria vya utendaji ambavyo vitatumika kupima utendaji na huduma zitolewazo kwa watu;

x Kuwepo utaratibu madhubuti wa kupata, kuchambua, kutafsiri, na kupeleka uchambuzi wa taarifa za utendaji kwa taasisi husika; na

xi Kutekeleza kwa wakati mapendekezo yaliyotolewa na kutoa mrejesho kwa taasisi husika.

*Usimamizi wa ufuatiliaji katika sekta ya umma*

xii Kubuni mfumo wa ufuatiliaji kwa namna ambayo taarifa zitakusanywa, kuchunguzwa, kujumlishwa na kutumika ipasavyo ili kuongoza na kujifunza ufumbuzi wake;

xiii Kubuni mfumo wa ufuatiliaji utakaotoa mwongozo wa mtiririko wa taarifa kwa ufanisi kati ya taasisi na ngazi mbalimbali za utawala ili kurahisisha utoaji wa maamuzi;

xiv Kupitia mara kwa mara na kuhuisha zana zinazotumika kufuatilia wigo wa tathmini ili kutoa mtazamo sahihi wa maendeleo ya kiidara ambao unaweza kutumika katika usimamizi, uwajibikaji, na mchakato wa kutathmini mfumo;

xv Kutoa mwongozo wa wazi wa kufuatilia utendaji wa idara katika matumizi ya rasilimali ili tathmini itakayofanywa itoe picha halisi ya kile kinachotokea;

xvi Kupeleka taarifa zinazopatikana katika mfumo wa tathmini kwa watumiaji sahihi ili kurahisisha hatua zinazopaswa kuchukuliwa;

xvii Kubaini mara kwa mara mapungufu ya mawasiliano na kuhakikisha taarifa zinawasilishwa kwa wakati muafaka na kwa walengwa kwa ajili ya kuchukua hatua za kiutawala na kiusimamizi.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Ukaguzi

Ukaguzi wa Ufanisi ni muhimu kwa sababu unalenga kuboresha uwajibikaji na utendaji wa taasisi za Serikali ili wananchi wapate huduma zinazolingana na thamani ya fedha ziliyotumika. Vigezo kadhaa hutumika kuchagua maeneo yanayolengwa na Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu. Miongoni mwa mambo hayo ni malalamiko kutoka kwa wananchi na umuhimu wa eneo linaloangaliwa pamoja na sababu za kijamii na kiuchumi.

Ukaguzi wa Ufanisi unatathmini ili kufahamu iwapo shughuli, mipango, au miradi inayohusisha rasilimali za umma katika Wizara, Idara, Serikali za Mitaa na Mashirika yote ya umma imesimamiwa kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi. Uwekevu, tija na ufanisi unaweza kuelezwa kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Uwekevu | - | Kupunguza gharama za rasilimali zinazotumika katika shughuli huku kukizingatiwa ubora sahihi. |
| Ufanisi | - | Uhusiano kati ya matokeo, kwa kuzingatia bidhaa, huduma, matokeo na rasilimali zilizotumika kuzalishia. |
| Tija | - | Kiwango ambacho malengo yamefikiwa na uhusiano kati ya malengo yaliyokusudiwa na matokeo halisi katika shughuli husika. |

## 1.2 Mamlaka ya Kukagua

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kisheria ya kufanya Ukaguzi wa Ufanisi kupitia Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008. Kifungu cha 28 cha Sheria hii kinasema “Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa lengo la kuthibitisha uwekevu, tija na ufanisi katika matumizi ya fedha au rasilimali za taasisi ya umma, anaweza kukagua, kuchunguza na kutoa ripoti, kadri atakavyoona inafaa kuhusu:

(a) Matumizi ya fedha na rasilimali za umma katika wizara, idara, mamlaka za serikali za mitaa, na mamlaka nyingine za serikali;

(b) Utekelezaji wa majukumu ya maofisa masuuli, wakuu wa idara, na wakuu wa taasisi mbalimbali za umma;

(c) Utekelezaji wa matakwa ya sheria ya mazingira, kanuni, na sera ya ndani ya mazingira na viwango.

Ukaguzi unafanyika kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa ufanisi. Viwango hivyo vinataka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kupanga na kutekeleza ukaguzi ili kupata ushahidi wa kutosha ambao utakuwa kigezo cha kuripoti mapungufu yaliyoonekana na kutoa hitimisho kwa kuzingatia lengo la ukaguzi husika.

## 1.3 Madhumuni ya Ripoti

Ripoti hii ya jumla inalenga kuwapa taarifa muhimu waheshimiwa wabunge, vyombo vya habari, umma pamoja na wadau wengine ili waweze kufanya maamuzi yatakayoongeza uwekevu, tija na ufanisi katika shughuli za serikali. Mwisho, muhtasari wa kila ripoti unatolewa kwa kubainisha mambo yatakayojadiliwa na Kamati za Kudumu za Bunge kwa kushirikisha maofisa masuuli wakati wa kusikiliza hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
Ripoti hii haikusudii kuwa mbadala wa ripoti sita za Ukaguzi wa Ufanisi ambazo zimefupishwa katika sura zinazofuata. Ili kuweza kupata uelewa wa kina wa mada mahsusi zilizojadiliwa katika ripoti hii, msomaji anashauriwa kusoma ripoti binafsi zilizokamilika. Ripoti hizo ni za Ukaguzi za Ufanisi katika maeneo yafuatayo:

- Utoaji wa Huduma za Ugani kwa Wakulima;
- Usimamizi wa Milipuko ya Magonjwa na Wadudu waharibifu wa Mimea;
- Udhibiti wa Usafi kwenye Maeneo ya Kuzalishia Nyama;
- Mfumo wa Udhibiti wa Ubora wa Elimu;
- Usimamizi wa Mchakato wa Tathmini ya Athari za Kimazingira; na
- Usimamizi wa Mikataba katika Taasisi za Umma.

## 1.4 Lengo Kuu la Ripoti

Ripoti hii imelenga kuonesha masuala yanayohusu utendaji wa serikali katika maeneo makuu matatu yafuatayo:

- Usimamizi wa data kwenye taasisi za serikali;
- Upimaji wa utendaji katika sekta ya umma; na
- Ufuatiliaji wa utendaji wa serikali.

Ripoti hii inatoa mchanganuo wa masuala yaliyobainika kwenye ripoti sita za ukaguzi wa ufanisi ili kuonesha mapungufu katika maeneo makuu matatu. Mwisho inapendekeza namna ya kuboresha mapungufu hayo.

## 1.5 Mchakato wa Uthibitisho wa Takwimu

Wizara, Idara, mashirika, taasisi na wakala mbalimbali wa Serikali waliokaguliwa walipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni yao juu ya matokeo ya ukaguzi na kusahihisha makosa yaliyojitokeza katika rasimu ya taarifa hii.

## 1.6 Muundo wa Ripoti

Ripoti hii ya jumla ina sura saba kama ifuatavyo:

**Utangulizi wa Ukaguzi wa Ufanisi**

Sura ya kwanza inatoa utangulizi wa ukaguzi wa ufanisi, mamlaka ya ukaguzi, madhumuni ya ripoti ya jumla, mchakato wa uthibitisho wa takwimu. Sura ya pili inatoa muhtasari wa muundo wa upimaji wa utendaji, ufuatiliaji na usimamizi wa data kwenye taasisi za umma.

**Kaguzi Zilizofanyika na Udhaifu Unaofanana**

Sura za tatu hadi tano zinatoa matokeo ya ukaguzi kwenye maeneo makuu matatu yafuatayo: upimaji wa utendaji, ufuatiliaji ili kubaini utekelezaji wa mapendekezo ya masuala yaliyobainka kwenye uchunguzi unaofanywa na taasisi husika, tathmini na ufuatiliaji wa shughuli mbalimbali za serikali; na usimamizi wa mifumo ya taarifa kwenye taasisi za umma.

Mchanganuo wa maeneo hayo ni kama ifutavyo: Sura ya tatu inaonesha udhaifu unaofanana kwenye eneo la *Usimamizi wa Data* kwa ripoti zote sita za kaguzi zilizofanyika; sura ya nne inaonesha udhaifu unaofanana kwenye eneo la *Upimaji wa Utendaji* kwenye ripoti zote sita za ukaguzi; na sura ya tano inaonesha mapungufu yanayofanana kwenye *Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali* kama ilivyobainishwa katika ripoti zote sita za ukaguzi.

**Hitimisho la Jumla na Mapendekezo**

Sura za sita na saba zinatoa mahitimisho ya jumla na mapendekezo ya masuala yaliyobainishwa katika maeneo makuu matatu kama yalivyotajwa hapo juu.

# SURA YA PILI

# USIMAMIZI WA UTENDAJI KATIKA TAASISI ZA UMMA

## 2.1 Utangulizi

Kufikia malengo ya programu ni muhimu katika kufanikisha programu yoyote ya umma. Ukusanyaji wa data ili kuonesha mafanikio ya programu ni muhimu kwa upimaji wa utendaji. Sura hii ya usimamizi wa utendaji inalenga kuonesha namna taasisi za umma, zinavyosimamia utendaji wake kupitia usimamizi wa data, upimaji wa utendaji na ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa shughuli zake.


Kwa kupima utendaji na kufanya ulinganifu wa utendaji huo, taasisi inaweza kupata taarifa zitakazosaidia kuongeza ubora, utoaji, gharama, na muda wa huduma. Data nzuri zinasaidia katika kufanya tathmnini ya utendaji wa taasisi za umma. Hii inaweza kufikiwa kupitia mbinu sahihi za ufuatiliaji wa utekelezaji utakaohakikisha malendo ya taasisi yanafikiwa kwa urahisi. Kwa hiyo, sura hii inatoa maelezo kuhusu uhusiano uliopo kati ya mfumo wa usimamizi wa data, usimamizi wa utendaji, na ufuatiliaji wa masuala ya kiutendaji katika taasisi za umma.

## 2.2 Usimamizi wa Data

Usimamizi wa Data unahusisha shughuli zote zinazohusu upangaji, utekelezaji, na, utekelezaji na uratibu wa mifumo kwa ajili ya upatikana, utunzaji, ulinzi, ukokotaji, usambazaji, uhifadhi, na namna ya kuharibu data.

Data zilizosimamiwa vizuri ni kielelezo kizuri na madhubuti cha masuala ambayo serikali imeahidi, imeweza kutekeleza, nini inafanya, na jinsi inavyotumia fedha za umma. Usimamizi wa data ni jukumu muhimu katika usimamizi wa taarifa. Data sahihi na zinazohusika ni chanzo cha taarifa muhimu. Kwa kusimamaia data kwa umakini, maamuzi sahihi ya kiutendaji yanaweza kufanyika. Ni dhahiri kuwa mafanikio ya kitaasisi hayategemei tu uwepo wa rasilimali bali pia matumizi madhubuti katika kufikia malengo yaliyopangwa. Hivyo, taarifa zinaweza kuchukuliwa kuwa ni kiungo muhimu kinachoshikamanisha taasisi. Data katika taasisi za umma, pamoja na mazingira yaliyopo, ni sehemu ya mkakati na mpango wa uendeshaji wa taasisi. Pamoja na mazingira yaliyopo, ni sehemu ya mikakati, mbinu na uendeshaji wa taasisi.

**Kielelezo 2.1 Usimamizi wa taarifa unavyohusishwa na mafanikio ya taasisi**




**Chanzo: Uchambuzi wa mkaguzi kususu mfumo wa ufafafnuzi**

Inajulikana kwamba umuhimu wa taasisi za umma inategemea kiwango cha taasisi katika wajibu wake unaotarajiwa . Kama ilivyooneshwa katika **Kielelezo 2.1** hapo juu, kufikiwa kwa malengo ya kitaasisi kunategemea maamuzi sahihi yaliyofanywa na maofisa husika. Taarifa nzuri inatokana na ubora wa taarifa zilizoandaliwa na kuhakikiwa baada ya kuandaliwa. Maamuzi sahihi yanaweza kufanywa iwapo tu mhusika ana taarifa sahihi.

## 2.3 Upimaji wa Utendaji kwenye taasisi za umma

Upimaji wa utendaji katika taasisi za umma unalenga katika uanzishaji wa mfumo wa kiutendaji, utambuzi, na uteuzi wa viashiria vya utendaji. Unalenga pia kuandaa mazingira ya viashiria vya utendaji na uendelezaji wa mipango na upimaji wa utendaji. Halikadhalika unalenga kufuatilia na kufanya tathmini ya taarifa za utendaji, ufafanuzi wa taarifa za kiutendaji, hatua za kuchukuliwa na utoaji wa marejesho.

Sekta za umma zinakabiliwa na changamoto kubwa ya kuongeza kiwango cha utoaji wa huduma kwa wananchi, na pia kuongeza ufanisi na tija katika ukusanyaji na utumiaji wa rasilimali zilizopo. Ili kuyafikia haya, utekelezaji makini wa utendaji katika taasisi za umma ni muhimu. Upimaji wa utekelezaji wa utendaji unatumia taarifa za kifedha na zisizo za kifedha.

Upimaji wa utendaji wa kifedha unajumuisha fedha zilizowekewa bajeti na zinazotumika. Upimaji wa utendaji unazingatia bajeti na idadi ya maombi ya ukaguzi yaliyotolewa, ubora wa utoaji huduma, kuwaridhisha wananchi, upatikanaji wa utoaji huduma, kuwaridhisha wafanyakazi, uvumbuzi wa huduma mpya zitolewazo, na uendelevu wa huduma zitolewazo. Inadaiwa kwamba upimaji wa utendaji unaweza kusaidia taasisi za umma kuongeza uwazi, kutoa njia ya kuzawadia utendaji bora, na kukuza kujifunza ndani na baina ya taasisi husika.

## 2.4 Ufuatiliaji wa utekelezaji katika tasisi za umma


Ufuatiliaji unaweza kufafanuliwa kuwa ni Ufuatiliaji wa Tathmini za Athari za mipango/ Miradi na mawasiliano kuhusu ufanisi wa Miradi/Mipango inayotekelezwa na taasisi za umma. Ufuatiliaji mzuri unaweza kusaidia mambo mengi ikiwemo kuthibitisha na kudhibiti shughuli za utekelezaji wa miradi. Mrejesho kutoka kwenye programu za ufuatiliaji pia unatoa fursa kwa wasimamizi wa miradi na vyombo vya udhibiti kutoa majibu mabadiliko yanapotokea.

Shughuli nyingi zinazohusika katika miradi zinaweza kuwa katika mbinu za kisayansi. Baadhi ya ufuatiliaji wa shughuli hutoa tathmni ya matumizi ya ufanisi wa majukumu haya. Ufuatiliaji unatoa uelewa mzuri wa teknolojia na mbinu mpya za kiutendaji. Hivyo, ufuatiliaji kunaboresha ubora wa hatua au mbinu zinazoweza kutumika katika miradi ya baadaye. Mipango ya ufuatiliaji inaweza kuboresha uelewa wa umma kuhusu madhara au matokeo halisi ya miradi ya maendeleo, hivyo kupelekea umma kuyakubali mapendekezo husika.

Ufuatiliaji madhubuti unahitaji kupangwa na kufanyika kwa wakati. Matokeo na utendaji yanapaswa kuhusisha wadau mbalimbali wa kisekta kama inavyoonekana kwenye.

Pia ufuatliaji unapaswa kuzingatia utendaji na uwasilisi wa wadau kama inavyooneshwa katika **Kielelezo 2.2**

**Kielelezo 2.2: Mfumo wa ufuatiliaji**




**Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kuhusu ufafanuzi wa mfumo**

Mawasiliano hayahitaji kusubiri kuandaliwa kwa taarifa husika ya tathmini ili kuweza kuwasilisha matokeo ya tathmini. Mpango tathmini unatakiwa uwe na mfumo wa kuweza kugawana matokeo ya awali ili kuwezesha marekebisho ya mpango na kufanya maamuzi.

## 2.5 Uhusiano kati ya usimamizi wa taarifa, upimaji wa utekelezaji, na ufuatiliaji wa utekelezaji

Katika utoaji wa huduma za umma, usimamizi wa taarifa ni muhimu sana katika kuboresha utendaji. Hii inajumuisha ukusanyaji, ufuatiliaji, upembuzi, wa kutafsiri, pamoja na kufanyia kazi taarifa za taasisi kwa ajili ya hatua maalumu. Upimaji wa michakato na matokeo ni mkabala madhubuti na utaratibu muhimu wa usimamizi wa taarifa. Pia unahusisha upimaji, usimamizi, pamoja na ufuatiliaji wa utendaji unaoendelea. Inasaidia taasisi kutambua na kutekeleza mipango kwa ajili ya maboresho ya mfumo wa utoaji wa huduma za umma na

kufuatilia utekelezaji wake[1] . Uhusiano kati ya vipengele hivi vitatu unaoneshwa katika **Kielelezo 2.3.**

**Kielelezo 2.3 Uhusiano kati ya taarifa, upimaji wa utendaji, na matokeo ya taarifa**




**Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kuhusu ufafanuzi wa muundo**

[1] Usimamizi wa data ili kuboresha utendaji. Idara ya Afya, rasilimali za huduma za afya ya Binadamu na usimamizi wa utoaji huduma, Marekani, Aprili 2011

**SURA YA TATU**

**USIMAMIZI WA DATA KWENYE SEKTA YA UMMA**

## 3.1 Utangulizi

Usimamizi wa data katika sekta ya umma unajumuisha shughuli zote zinazohusu mipango, maendeleo, utekelezaji na usimamizi wa mifumo yaupatikanaji, uhifadhi, usalama, urejezaji, usambazaji, utunzaji na njia za kuharibu data.

Usimamizi mzuri wa data hutoa ushahidi wa wazi na wa kudumu kuhusu ahadi za serikali, nini ilichokifanya, huduma inazozitoa, na jinsi inavyotumia fedha za umma. Udhaifu katika udhibiti wa kumbukumbu unaweza kusababisha uwezekano wa upotoshaji wa taarifa na hivyo kutoa fursa za udanganyifu, rushwa na ubadhirifu. Pia hudhoofisha uwezo wa wananchi kudai haki na stahili zao; hudhoofisha uwezo wa kupangana kufuatilia sera na huduma; na husababisha ugumu katika kupata taarifa za umma kwa ufanisi[2]

Wakati wa ukaguzi wa ufanisi uliofanywa katika maeneo sita ya kiukaguzi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilibaini maeneo ambayo yameonyesha udhaifu katika usimamizi wa data miongoni mwa taasisi za serikali. Mapungufu haya yameelezwa kama ilivyoainishwa hapa chini.

## 3.2 Malengo ya usimamizi wa data kwenye sekta ya umma

Malengo ya jumla ya Sura hii ni kutathmini jinsi taasisi za serikali zinavyosimamia matumizi ya taarifa wakati zikitekeleza majukumu yake. Taasisi hizi pamoja na nyinginezo ni zile ambazo zimetolewa katika ripoti za ukaguzi wa ufanisi kama zilivyoainishwa kwenye Sura ya Kwanza ya ripoti hii. Hususani, lengo la kaguzi hizi lilikuwa ni:

[2]ISO 30300:2011: Taarifa na uhifadhi wa nyaraka – Mifumo ya Usimamizi wa Kumbukumbu – Nyaraka kuu na Msamiati, www.iso.org/iso/catalogue_detail?csnumber=53732

- Kufanya tathmini ya kiwango ambacho taasisi za serikali zinasimamia data katika kutatua mapungufu ya kiutendaji katika kazi zao ili kuongeza tija na ufanisi katika shughuli, miradi, na mipango ya serikali.

- Kutambua mapungufu katika usimamizi wa data na hivyo kutoa mapendekezo ambayo yataongeza thamani na tija na kusaidia kutatua mapungufu hayo.

Ni vigumu kutambua tija na ufanisi wa shughuli za serikali kwa sababu ya mapungufu ya usimamizi wa data ambayo yamekuwa yakionekana katika kaguzi nyingi zilizofanyika. Mapungufu katika maeneo yote yaliyotambuliwa yanahusiana na hivyo kuathiriana. Mapungufu hayo yameelezwa katika sehemu zifuatazo hapa chini.

## 3.3 Uandaaji na uzalishaji wa data

Taasisi za serikali zinatarajiwa kuwa na mifumo maridadi ya kupokea na kupokea data ili kuziwezesha kupokea, kupata na kuzalisha data sahihi na muhimu kwa taasisi husika. Katika taarifa sita za ukaguzi wa thamani, ilibainika kuwa kulikuwa na mapungufu makubwa yanayohusiana na upokeaji, uandaaji na uzalishaji wa data. Taasisi za umma hazikuweza kupata data muhimu ambazo zingeziwezesha kuwa na taarifa muhimu juu ya utendaji na changamoto zinazozikabili.

### 3.3.1 Mapungufu katika upatikanaji wa data

Katika ukaguzi wa usimamizi wa milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea ilibainika kuwa Serikali za Mitaa zimewekewa Mfumo wa Upataji wa Data za Kilimo ambazo hurekodi taarifa za kilimo na ufugaji. Moja ya data hizo ni milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika (Wizara ya Kilimo) haikuweza kupokea data kutoka kwenye Halmashauri kwa sababu mfumo husika hautoi hali halisi ya milipuko ya magonjwa ya mimea kwa wakati husika. Hali hii imesababishwa na kutokuwepo kwa ufuatiliaji pamoja na ukosefu wa data kwa Wizara ya Kilimo ambazo zingesaidia kudhibiti milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea nchini.

Kwa upande mwingine, ukaguzi wa usimamizi wa mchakato wa tathmini ya athari za mazingira ulibainisha kuwa rejesta ya miradi iliyopo katika Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ilionesha kuwa jumla ya miradi 381 ikijumuisha miradi ya ujenzi ilisajiliwa kwa kipindi cha mwaka 2010/11 hadi 2014/15. Hata hivyo, kwa kipindi hichohicho, jumla ya miradi ya ujenzi iliyotekelezwa (kwa mujibu wa rejesta ya Bodi ya Makandarasi) ilikuwa 15,266. Hii inaashiria kuwa miradi ya ujenzi ipatayo 11,455 ambayo ni sawa na asilimia 75 ya miradi yote ya ujenzi inayotekelezwa haikusajiliwa au kufanyiwa tathmini. Kutofanyika tahimini kwenye miradi ya namna hii ni kinyume cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004.

Vilevile, hii imekwamisha kufanya maamuzi iwapo tathmini ya athari za mazingira ifanyike au la[3] . Hii inaashiria kuwa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira halikuweza kupata taarifa za kutosha na sahihi ambazo zingeweza kuathiri mipango yake ya usimamizi wa shughuli za mazingira.

### 3.3.2 Udhaifu katika uzalishaji na uhakiki wa data

Ukaguzi wa ufanisi wa udhibiti wa usafi katika uzalishaji wa nyama ulibaini mapungufu katika mifumo ya utoaji wa data baina ya Mamlaka ya Chakula na Dawa, Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi (Wizara ya Mifugo), na Ofisi ya Rais - TAMISEMI; Hii ilidhihirishwa na Wizara ya Mifugo kukosa taarifa muhimu kuhusu usalama wa nyama. Taarifa hizi zilipaswa kukusanywa na Mamlaka ya Chakula na Dawa kupitia shughuli zao za ukaguzi kwenye machinjio.

[3] Kanuni 10(2) & 11(3) Kanuni za tathmini ya athari za mazingira na ukaguzi za mwaka, 2005

Ilibainika pia uwepo wa udhaifu katika uratibu wa utendaji ndani ya Wizara ya Afya na baina ya Wizara ya Afya, na Mamlaka ya Chakula na Dawa umechangia Wizara ya Afya kushindwa kufuatilia utendaji wa Mamlaka ya Chakula na Dawa katika kusimamia hali ya usafi katika mchakato wa uzalishaji wa nyama kwa kutumia taarifa zinazozalishwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa na wizara za kisekta. Wakati wa mapitio ya taarifa za kila mwezi za robo mwaka, na za mwaka ilibainika kwamba taarifa zote hizi hazikulenga usafi wa nyama na hapakuwepo taarifa yoyote Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliyoonesha utendaji wa shughuli za huduma kwa mifugo kwenye Halmashauri mbali ya kuwepo kwa mratibu wa sekta hiyo katika halmashuri husika.

Ilibainika pia kuwa, Wizara ya Mifugo na Mamlaka ya Chakula na Dawa hazikuandaa wala kuzalisha data muhimu ambazo ziliendana na idadi ya machinjio yaliyosajiliwa. Mapitio ya taarifa ya mwaka ya Mamlaka ya Chakula na Dawa kuhusu usajili wa machinjio nchini yalibainisha kuwa asilimia 98 ya machinjio yanayofanya kazi hayakusajiliwa (ni machinjio 20 tu kati ya 932 ndiyo yaliyosajiliwa). Hii ilikuwa ni kinyume cha mahitaji ya Sheria ya Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Magonjwa ya Mifugo. Kwa maana hiyo, taasisi mbili hazikuwa na taarifa za idadi ya machinjio yaliyosajiliwa na yasiyosajiliwa.

**Jedwali 3.1: Makundi ya machinjio ambayo hayakusajiliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa na Wizara ya Mifugo**

| Kundi la Machinjio | Idadi ya machinjio yaliyopo | Asilimia ya machinjio yaliyosajiliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa | Asilimia ya machinjio yaliyosajiliwa na Wizara ya Mifugo |
|---|---|---|---|
| Machinjio ya kisasa | 11 | 100 | 27 |
| Machinjio ya kati | 85 | 26 | 0 |
| Karo la machinjio | 1094 | 0 | 0 |

**Chanzo: Mapitio ya hali ya usajili kutoka Wizara ya Mifugo na Mamlaka ya Chakula na Dawa pamoja ya uchambuzi wa Wakaguzi, 2016**

Jedwali 3.1 linaonesha kuwa kumekuwepo na mapungufu ya uzalishaji wa data kutoka Mamlaka ya Chakula na Dawa na Wizara ya Mifugo kuhusu idadi ya machinjio ya kisasa; machinjio ya kati; na karo za machinjio. Mapungufu yaliyoonekana yanahusu: kasoro katika kukusanya data zinazohusiana na machinjio yaliyosajiliwa, na utunzaji wa kumbukumbu na kupeana taarifa baina ya Wizara ya Mifugo, na Mamlaka ya Chakula na Dawa. Data hizi ni muhimu ili kuelewa idadi ya machinjio ambayo hayasimamiwi kwa sababu ya kutosajiliwa.

Baadhi ya taasisi zilizokaguliwa hazikuandaa kabisa data ambazo ni muhimu kama ambavyo ilibainika kwenye Ukaguzi wa Usimamizi wa Mfumo wa Udhibiti Ubora wa Elimu ambapo Wizara ya Elimu na Ufundi Stadi na Ofisi ya Rais-TAMISEMI hazikuweza kutoa taarifa juu ya utendaji na uendeshaji wa vituo vya walimu. Ofisi ya Rais-TAMISEMI ambayo inahusika na kusimamia na kufuatilia utendaji wa halmashauri ambazo, kwa kupitia maofisa elimu wa kata, wilaya, na waratibu wa vituo vya waalimu ina jukumu la kuhakikisha kuwa msaada unatolewa kwenye vituo vya walimu na kwamba walimu wanapata mafunzo, ilitakiwa kuandaa taarifa hizo ambazo zingeviwezesha vituo hivi kufanya kazi.

Kulikuwepo na matukio ambapo taasisi zilizokaguliwa hazikuweza kuhakiki data ambazo ilizitumia kuandaa nyaraka muhimu. Kwa mfano, Ukaguzi wa Usimamizi wa Miradi ya Ujenzi Mijini ulibaini kuwepo kwa mapungufu katika kuhakiki taarifa zilizotumika kuandaa makisio ya gharama "Makadirio ya Ujenzi". Ilionekana kuwa miundo ya miradi haikufanyika kikamilifu kwa sababu wahandisi washauri hawakukusanya taarifa muhimu wakati wa utafiti na uchunguzi wa udongo ili kuwezesha uandaaji wa taarifa zenye kina juu ya muundo wa miradi.[4]

[4] Kifungucha 39.1 chaVifungu vya Masharti ya Jumla

Kwa kutumia taarifa zilizokusanywa, wahandisi washauri walitakiwa kuandaa michoro iliyoonesha miundo na makadirio ya ujenzi ambayo inaonesha kiwango cha mahitaji ya kazi. Kuhusu hili, makisio halisi kwa kazi zote zilizopimwa zilitakiwa kuwemo kwenye makadirio ya ujenzi ili kuongoza shughuli za ujenzi. Mapitio ya maagizo ya mabadiliko yalionesha kuwa Makadirio ya Ujenzi kwenye fungu la F&H na Loti 3, 4 na 5 yalikosa mahitaji muhimu yaliyotakiwa kwenye kazi hivyo kusababisha kuwepo kwa umuhimu wa kuongezea mahitaji mengine ya ziada yaliyofikia kiasi cha shilingi bilioni 2,807.4.

Kwenye ukaguzi huohuo, ilibainika kuwa kwa kuzingatia mapungufu hayo hapo juu, gharama ya mkataba iliongezwa na Wizara ya Maji kinyume cha utaratibu. Kwenye loti 5 ya Mradi wa maji Chalinze, gharama ya mkataba iliongezeka hadi kufikia milioni 50.1 baada ya kuweka viwango vipya kwenye Makadirio ya Ujenzi ambavyo vingeweza kutekelezwa kwa gharama nyinginezo na viwango kwenye mkataba. Kwa kufanya hivyo, Wizara ya Maji ilienda kinyume cha kifungo cha 43.4 cha Vifungu vya Masharti ya Jumla.

Taarifa zilizokusanywa na kuhakikiwa zilikuwa muhimu kutumika kama muongozo au ulinganishaji wakati wa utekelezaji wa miradi. Katika ukaguzi wa usimamizi wa mikataba ya miradi ya ujenzi ya maji mijini, ilibainika kuwa mipango kazi ambayo ilikuwa muhimu katika kusaidia kuongoza utekelezaji wa miradi husika haikupitiwa wala kuhuishwa mara kwa mara kama ilivyotakiwa kwenye mikataba husika.

Kwa mfano, katika mradi wa maji wa Musoma ambao gharama yake ya awali ilikuwa shilingi bilioni 40.597, ilibainika kuwa taarifa ya maendeleo ya mradi ya robo mwaka ya Februari 2013, Wizara ya Maji ilimwandikia mkandarasi kumjulisha mabadiliko kwenye gharama ya mradi ambao awali ulionekana kuthaminiwa kwa kiasi cha chini kwa sababu ya makosa ya kimahesabu kwenye Makadirio ya Ujenzi. Kwa sababu hii gharama ya mkataba iliongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 27.602 hadi kufikia shilingi bilioni 40.624. Kushindwa kuhuisha mkataba kwa wakati kulisababisha ugumu katika usimamizi kwa kuwa mhandisi hakuweza kutumia mipango kazi iliyopitiliza muda wake.

Ilibainika pia kwenye ukaguzi huohuo kuwa kulikuwepo na upungufu katika kuandaa na kuhakiki mikataba. Mapitio ya mikataba yalibainisha kuwa kulikuwepo na makosa katika kuweka namba katika mikataba ambapo mikataba iliwekwa namba moja kwenye miradi miwili tofauti na kuwepo kwa namba mbili za mkataba katika mradi mmoja. Taarifa muhimu kama vile tarehe za kusaini mkataba, kukabidhi eneo la kazi, kuanza, na kukamilisha kazi vilinakiliwa tofauti katika viambatanisho/nyongeza ya mkataba.[5]

Kulikuwepo na taarifa mchanganyiko zilizohusu aina ya dhamana ya utendaji ambayo ingetolewa na mkandarasi wa fungu F&H la mradi wa ujenzi. Hata hivyo, hapakuwepo uainishaji wa majukumu baina ya msimamizi wa mradi aliyetajwa kwenye mkataba na mhandisi mshauri ambaye aliajiriwa kusimamia mradi huo. Hii ilisababishwa na maandalizi hafifu ya mradi na hivyo kushindwa kufanya mapitio ya mkataba (jambo lililosababishwa na Wizara ya Maji) kabla ya kusaini mkataba ili kuhakikisha vipengele na masharti ya mkataba vinaeleweka kwa pande zote mbili zinazohusika na mkataba.

### 3.3.3 Mapungufu ya data kwa ajili ya kufanya maamuzi

Ilibainika kuwa dataambazo zilizalishwa na taasisi za serikali hazikuzingatia mambo muhimu ambayo yangewezesha mamlaka husika zichukue maamuzi sahihi. Kwa mujibu wa kanuni za tathmini za athari za mazingira[6] , taarifa ya athari za mazingira inatakiwa kuzingatia kuidhinisha miradi ambayo inajengwa kwenye maeneo hatarishi kimazingira kama vile sehemu oevu na sehemu zenye mitiririko ya maji. Vilevile, kanuni zinaitaka Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kufanya mapitio ya taarifa ya tathmini ya athari za mazingira kwa kuzingatia vigezo vinne[7] .

---

[5] Zingatia kiambatanisho cha 12 cha Taarifa ya Ukaguzi kuhusu Usimamizi Mikataba ya Miradi ya .Maji Mijini

[6] Kanuni za tathmini ya athari na ukaguzi wa mazingira , 2005

[7] maelezo ya uendelezaji wa mazingira, masharti ya awali, kutambua na kutathmini madhara mahususi, njia mbadala, namna ya kukabili madhara, mango wa kimazingira, jinsi ya kutekeleza, uhusika wa wadau pamoja na uwasilishaji wa matokeo.

Hata hivyo ilibainika kuwa tathmini ya athari za mazingira kwa ajili ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi haukuzingatia vigezo hivyo muhimu ikiwa ni pamoja na kutambua na kutathmini athari za kimazingira na hatua za kuyakabili katika bonde la mto Msimbazi ambayo yangetokana na ujenzi wa kituo cha maegesho ya magari ya mradi huo katika eneo la Jangwani. Kutokana na taarifa za kiupotoshaji zilizokuwa kwenye taarifa ya tathmini ya athari za mazingira ambayo iliwasilishwa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kuidhinishwa, eneo hilo ambalo linajulikana kwa kuwa na matatizo ya mafuriko ya mara kwa mara, lilikumbwa na mvua kali na mtirirko wa maji iliyosababisha maji kujaa na kutiririka juu ya daraja la Jangwani na katika makazi ya watu na kuathiri sehemu ya miundombinu ya mradi huo.

## 3.4 Uhifadhi wa kumbukumbu

Taasisi zilizokaguliwa zinatarajiwa kutunza ubora wa data zinazozalishwa ilimradi tu ni muhimu na zinafaa kwa shughuli na utendaji katika majukumu yao. Vivyo hivyo, mifumo inatakiwa kuwepo ili kuwezesha taasisi hizo kupata taarifa kutoka vyanzo mbalimbali kwa matumizi mbalimbali. Ukaguzi uliofanyika ulibaini kuwepo mapungufu ambayo yaliathiri malengo ya taasisi katika eneo la utunzaji wa kumbukumbu kama inavyoelezwa hapa chini.

### 3.4.1 Ukosefu wa mifumo ya kukusanya na kuhifadhia data (data za awali)

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwepo na udhaifu katika utunzaji wa taarifa kwenye taasisi zilizokaguliwa. Katika baadhi ya maeneo, taarifa zilizotarajiwa kuandaliwa na kuhifadhiwa na taasisi zilizokaguliwa hazikuweza kutolewa kwa wakaguzi baada ya kuhitajiwa.

Kwa mfano, katika ukaguzi wa usimamizi wa huduma za ugani, ilibainika kuwa halmashauri zilikosa rejesta za kuhifadhi kumbukumbu za shughuli za kilimo "daftari la kilimo". Daftari la kilimo ni shajara ambayo inatumiwa na maofisa ugani wa kata na vijiji katika kutunza kumbukumbu za shughuli za kilimo kila siku. Kwa kawaida shajara hiyo ina namba za idadi ya wakulima waliofikiwa na huduma za ugani; aina ya mazao yanayolimwa; na ratiba ya kazi ambayo inaonesha shughuli zote zilizofanywa na maofisa hao kila siku.

Mahojiano yaliyofanywa baina ya wakaguzi na maofisa kutoka halmashauri yalibainisha kuwa madaftari ya kilimo hayakuwepo kwenye halmashauri. Hii ni kinyume cha miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za ugani kwa wakulima ambayo inamtaka kila ofisa ugani katika ngazi ya kata na kijiji kuweka kumbukumbu za shughuli za ugani na kilimo kwa kutumia daftari la kilimo.

Ukosefu wa taarifa ulisababishwa na Wizara ya Kilimo kushindwa kupeleka madaftari ya kilimo kwenye halmashauri na hivyo maofisa ugani wengi hawajawahi kuziona. Vilevile, taarifa za jumla za mwaka zilitolewa mbele ya kamati ya kilimo ambayo hukutana kila baada ya miezi minne ili kupitia maendeleo ya shughuli za kilimo na kufanya maamuzi. Mambo yaliyojitokeza kwenye mikutano hiyo yalitakiwa kuwasilishwa kwenye Halmashauri (kama mrejesho) kupitia Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Ofisi ya Rais-TAMISEMI ilikiri kufanya hivyo kwa kupitia warsha na semina. Hata hivyo hapakuwepo na taarifa zozote za warsha wala semina ambazo zililenga halmashauri kuthibitisha hojaya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Katika Ukaguzi wa Usimamizi wa Udhibiti wa Usafi katika Uzalishaji wa Nyama, wakaguzi kwa kufanya mapitio ya taarifa za ufuatiliaji na tathmini za mifugo na kilimo kutoka Ofisi ya Rais-TAMISEMI hawakuweza kubaini taarifa yoyote iliyokusanywa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kutoka kwenye halmashauri iliyobainisha utendaji wa halmashauri katika kuhakikisha inazalisha nyama iliyo salama kwa ajili ya matumizi ya umma. Matokeo yake, Ofisi ya Rais-TAMISEMI haifahamu kiwango cha uchafuzi kinachofanywa wakati wa mchakato wa kuzalisha nyama na hakuna hatua zilizochukuliwa kwa ajili ya kuepusha hali hiyo ili kutunza afya za walaji. Hii imesababishwa na halmashauri kutotunza data za machinjio yanayotumika kwenye maeneo yao.

Wakati wa ukaguzi huo, mahojiano baina ya wakaguzi na maofisa wa kanda wa Sumbawanga na Mwanza yalibaini kuwa maofisa hao hawakuwa na data za idadi ya machinjio ambayo hutoa taarifa za kila siku kuhusu magonjwa ya mifugo. Wizara ya Mifugo haikufanya uchambuzi na kukusanya taarifa zilizotoka kwenye vituo vyake vya kanda. Hivyo basi, wakaguzi hawakuweza kuhakiki taarifa zilizokusanywa na Wizara ya Mifugo kwa kuwa hapakuwepo data za jumla kutoka kwa sekta zinazotakiwa kutoa taarifa Wizara ya Mifugo.

### 3.4.2 Udhaifu katika mifumo ya kurekodi data

Ukaguzi ulibaini mapungufu katika eneo la kurekodi data hasa kutunza kumbukumbu ambazo zinatekelezwa na taasisi husika. Katika Ukaguzi wa Usimamizi wa Udhibiti wa Usafi kwenye mchakato wa uzalishaji nyama, ilibainika kuwa kati ya machinjio kumi na mbili (12) yaliyotembelewa, machinjio matano[8] (5) hayakuwa na kumbukumbu za ukaguzi wa awali wa wanyama. Hii iliashiria kuwepo kwa uwezekano wa kutokufanyika ukaguzi wa awali kinyume cha kanuni ya 6 (2)(h) ya Kanuni za Wanyama za Mwaka 2011 na Tangazo la Serikali na. 359 ambalo linawataka wakaguzi kuweka kumbukumbu za ukaguzi na kutoa taarifa kila mwezi. Wakaguzi walibaini kwamba wakaguzi wa wanyama walikagua kati ya wanyama 300 kwa usiku mmoja bila ya kuwa na kitabu cha kuchukulia taarifa za awali kama inavyotakiwa ili kusaidia wakaguzi wa nyama kutunza kumbukumbu na kuandaa taarifa na hivyo kusababisha kuwepo kwa hatari ya kupata taarifa zisizo sahihi kuhusu magonjwa yanayobainishwa wakati wa ukaguzi baada ya uchinjaji.

Vilevile, ilibainika kuwa kwenye machinjio 12 yaliyotembelewa, machinjio 8 hayakuwa na taarifa juu ya upimaji wa afya kwa watumishi wa machinjio kinyume cha sheria ya Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Usafi wa Chakula ya Mwaka 2006, kanuni ya 7(b). Kanuni hizi zinataka watumishi kupimwa afya kabla ya kuajiriwa katika muda wa angalau kila baada ya miezi sita na majibu ya upimaji huo yatunzwe katika ofisi za machinjio husika. Hata hivyo, ilikuwa vigumu kufahamu idadi kamili ya wafanyakazi waliopimwa na ambao hawakupimwa afya kwa sababu kumbukumbu kuhusu upimaji wa afya na idadi ya watumishi hazikupatikana kwenye ofisi hizo.

[8]. Lufaveso, Ukonga, Kiboroloni, Moshi na Uyole

Ilibainika pia katika Ukaguzi wa Udhibiti wa Ubora wa Elimu kuwa ongezeko la uandikishaji lilikuwa ni matokeo ya programu za Serikali za elimu ambazo ziliongeza changamoto kwenye mahitaji na usambazaji wa walimu. Hii ilisababisha Serikali kuamua kutoa leseni za kufundishia kwa wahitimu wa kidato cha sita na kwamba wangepewa mafunzo ili kuwa walimu kamili ndani ya miaka miwili hadi mitano kama ilivyoainishwa kwenye mikataba yao.

Uchambuzi wa data kutoka Idara ya Huduma za Ualimu katika Wizara ya Elimu ulibaini kuwa walimu waliopewa vibali vya kufundisha na ambao walitakiwa kujiendeleza hadi kufikia walimu kamili hawakufanya hivyo kwa kipindi cha miaka kumi. Kwa kuzingatia hilo, data zinaonesha kuwa kuna walimu 405 ambao hawakujiendeleza kwenye taaluma ya ualimu. Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa kulikuwa na zaidi ya walimu 88 waliokuwa na kibali cha ualimu ambao walijiendeleza kwenye taaluma tofauti na ualimu na walimu 317 ambao huenda hawakujiendeleza kwenye taaluma ya ualimu kwa kuwa taarifa zao hazikupatikana na hivyo kushindwa kuhakikiwa.

Pia, katika ukaguzi wa usimamizi wa magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea, mapitio ya mpango wa kati wa matumizi, Mpango Mkakati na Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kutoka kwenye Halmashauri ulibaini kuwa Halmashauri zilitoa taarifa za matukio ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea. Hata hivyo taarifa hazikujitosheleza kuhusu milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea. Kumbukumbu zilizowekwa na ofisi za kanda za Wizara ya Kilimo na halmashauri zilizotembelewa hazikuonesha mwenendo wa usambaaji wa wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea. Madhara yake ni kuwa juhudi kubwa zilielekezwa kwenye maeneo yenye milipuko kidogo kuliko ile yenye milipuko mikubwa.

### 3.5. Usahihi wa Data

Katika matumizi ya data, taasisi zilizokaguliwa zilitarajiwa kuandaa au kutumia taarifa halisi na sahihi. Kwenye ukaguzi wa Udhibiti wa Ubora wa Elimu, wakaguzi walifanya uchambuzi wa uwepo wa walimu wasio na sifa. Uchambuzi wa taarifa zilizopatikana kutoka

Taarifa ya Taifa ya Takwimu ya Elimu na Ofisi ya Rais-TAMISEMI ulionesha ongezeko kubwa la idadi ya walimu wasiokuwa na sifa kwa mwaka 2014 kinyume na miaka miwili iliyopita ya 2012 na 2013 na punguzo kubwa kwa mwaka 2015.

Kwa mujibu wa maofisa kutoka Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kupungua kwa idadi ya walimu wasio na taaluma kulisababishwa na maamuzi ya serikali kuajiri walimu waliokuwa na sifa na wale waliokuwa kwenye ajira walijiendeleza na kuwa na sifa za ualimu baada ya kumaliza programu za mafunzo.

Serikali ilikuwa ikigharimia programu za mafunzo ya kitaaluma kwa ajili ya walimu ili kuhakikisha walimu wote ambao hawakuwa na sifa wanakuwa na sifa. Vilevile, idadi ya walimu wasio na sifa ilipungua kwa vile baadhi ya waalimu ambao hawakuwa na sifa waliamua kustaafu bila kujiendeleza. Hata hivyo, ongezeko la idadi ya walimu ambao hawakuwa na sifa haikuweza kupatiwa maelezo kwa sababu ya kumbukumbu zisizo sahihi zilizopatikana kutoka kwenye Taarifa ya Taifa ya Takwimu za Elimu.

Wakati huohuo Ukaguzi wa Usimamizi wa Mikataba ya Miradi ya Ujenzi Mijini ilibainika kuwa mipango kazi ya miradi haikufuatwa wala kuhuishwa kama ilivyotakiwa na masharti ya mkataba[9] Kwa mujibu wa mikataba, mipango kazi iliyoonyesha taratibu za kazi, mipangilio, amri na muda kwa shughuli zote za kazi ilitakiwa kuhuishwa kila baada ya siku ishirini na nane. Hata hivyo, ilibainika kuwa makandarasi katika miradi yote iliyofanyiwa mapitio na wakaguzi, walikuwa nyuma ya muda nje ya mipango kazi ambayo ilikuwa haijahuishwa [10] [11] [12] [13]

[9] Kifungu cha 29.1 Vifungu vya Masharti ya Jumla kwenye mradi wa Chalinze na kifungu cha 8.3 cha miradi ya Bukoba na Musoma

[10] Rejea tamko la mwajiri wakati wa usuluhishi wa mradi wa F&H

[11] Barua yenye kumbukumbu namba: 10/TZ/CHA/03/10 of 15/1/2014.

[12] Dondoo za kikao cha mwezi Namba. 011 kilichofanyika tarehe 26 Machi 2014 (taarifa ya maendeleo robo mwaka Namba. 6

[13] Dondoo za kikao cha makubaliano Namba 023 .

**Jedwali 3.2: Makosa katika vitu vilivyokadiriwa na kuthaminiwa chini ya gharama halisi kwenye makadirio ya ujenzi**

| Fungu namba | Vitu vilivyothaminiwa kwa gharama ya chini (million TZS) | Vitu vilivyoachwa kwenye makadirio ya ujenzi (million TZS) | Jumla |
|---|---|---|---|
| Fungu la 2 | 1896.5 | 246.4 | 2142.9 |
| Fungu la 3 | 613.0 | 17.4 | 630.4 |
| Fungu la 4 | 218.0 | 36.1 | 254.1 |
| Fungu la 5 | 766.2 | 496.3 | 1262.5 |
| Fungu la 6 | 1215.9 | 452.1 | 1668.0 |
| Fungu la F &H | 1623.5 | 3207.9 | 4831.4 |
| Bukoba | 2003.2 | 416.6 | 2419.8 |
| Musoma | 2607.1 | 494.8 | 101.9 |
| **Jumla** | **10,943.40** | **5,367.6** | **16,311** |

**Chanzo: Maagizo ya mabadiliko na viambatisho vya mikataba**

## 3.6 Matumizi na Uwasilishaji wa Data

Ukaguzi kwa Jumla ulibaini mapungufu katika kushirikishana taarifa baina ya wizara za kisekta, idara za serikali, na halmashauri. Mapungufu haya yameelezwa katika sehemu zinazofuata hapa chini.

### 3.6.1 Mapungufu katika matumizi ya data wakati wa kuandaaa mipango kazi

Mipango ni moja ya shughuli muhimu ambapo taasisi husika huandaa mikakati ya shughuli zinazotarajiwa kupangwa katika mwaka wa fedha husika na inaweka namna ya kufikia mikakati hiyo. Katika uandaaji wa mipango, taarifa za miaka ya nyuma ni muhimu na inafaa katika kutathmini makadirio ya ukubwa wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka husika. Taasisi za serikali zilitarajiwa kuandaa mipango yake kutokana na taarifa zilizopita.

Mapitio ya nyaraka zilizohusu mipango ikijumuisha shughuli zilizofanyika ndani ya mwaka kwenye Usimamizi wa Mchakato wa Tathmini ya Athari za Mazingira yalibainisha kuwepo kwa tofauti kubwa baina ya shughuli zilizoanishwa kwenye mipango na zile zilizotekelezwa ambapo idadi ya tathmini ya athari za mazingira zilizopitiwa na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa muda wote zilikuwa na idadi kubwa zaidi kuliko zile zilizopangwa kwenye mwaka husika kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita (rejea Jedwali 3.3 hapo chini).

**Jedwali 3.3: Malengo na mafanikio ya upitiaji wa taarifa za tathmini ya athari za mazingira**

| Mwaka wa fedha | Idadi ya taarifa za tathmini ya athari za mazingira zinazotarajiwa kufanyiwa mapitio | Idadi ya taarifa zilizofanyiwa mapitio | Tofauti (asilimia) |
|---|---|---|---|
| 2010/2011 | 50 | 146 | 192 |
| 2011/2012 | 100 | 208 | 108 |
| 2012/2013 | 150 | 176 | 17 |
| 2013/2014 | 100 | 371 | 271 |
| 2014/2015 | 500 | 701 | 40 |

**Chanzo: Mipango ya Mwaka ya Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira 2010-2014 pamoja na Taarifa ya Mwaka**

Jedwali 3.3 linaonesha kuwa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira halikuwahi kujifunza kutokana na mwenendo wa taarifa za miaka ya nyuma kama inavyoonekana kwenye Jedwali 3.3. Kwa kipindi hicho, imekuwa ikiendelea kupanga idadi ya juu zaidi ya taarifa zilizofanyiwa marejeo (tathmini ya athari za mazingira). Malengo ya mapitio ya taarifa ya tathmini ya athari za mazingira yalizidi kuongezeka zaidi mwaka 2014. Hata hivyo, idadi ya taarifa ambazo zilifanyiwa mapitio ilibaki kuwa juu. Hii ilisababisha udhaifu katika mipango ya matumizi ya rasilimali na kusababisha mazoea ya kufanya mapitio ya dharura na hivyo kuwepo kwa ongezeko la marejeo ya dharura ambayo yanaongeza gharama ambazo hazikuwepo katika mipango ya awali ya mwaka.

### 3.6.2 Udhaifu katika kuwasilisha na kushirikishana data

Kulikuwepo na mapungufu katika uwasilishaji na ushirikishanaji wa data baina ya taasisi za serikali. Kwa mfano, katika Ukaguzi wa Udhibiti wa Afya katika Mchakato wa Uzalishaji wa Nyama, ilibainika kuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa na halmashauri hazikuwasilisha taarifa zao za ukaguzi kwa wadau ambao walitakiwa kupokea taarifa hizo (angalia Jedwali 3.4).

**Jedwali 3.4: Uwasilishaji wa taarifa za ukaguzi za Mamlaka ya Chakula na Dawa na Halmashauri kwa wadau**

| Taarifa za ukaguzi kutoka kwenye mamlaka | Wadau waliostahili kupata taarifa za ukaguzi | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wizara ya Mifugo | Wizara ya Afya | Halmas hauri | Mamlaka ya Chakula na Dawa | Sekretarieti za Mkoa | Ofisi ya Rais-TAMISEMI |
| **Mamlaka ya Chakula na Dawa** | Haikupok elewa | Haikup okelew a | Ndiyo | - | Ndiyo | Nadra |
| **Halmashauri** | Haikupok elewa | haikupo kelewa | | Ndiyo | Nadra | Nadra |
| **Sekretarieti za Mkoa** | haikupok elewa | Nadra | Nadra | Nadra | - | Nadra |

**Chanzo: Taarifa zilizowasilishwa na Uchambuzi wa Wakaguzi, 2015**

Hapakuwa na ushahidi ulioonesha kwamba halmashauri zilipeleka taarifa zao za ukaguzi Wizara ya Mifugo au Wizara ya Afya. Hii ilithibitishwa wakati wa mahojiano na maofisa kutoka Idara ya Huduma za Kinga ya Wizara ya Afya. Pia, halmashauri ziliwasilisha taarifa zao za matokeo ya ukaguzi kwa nadra kwenye Sekretarieti za Mkoa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wizara ya Mifugo, na Wizara ya Afya. Matokeo yake, mapendekezo yaliyotolewa na wakaguzi kwenye taarifa zao hayakutekelezwa ipasavyo na halmashauri husika.

Mfano mzuri wa athari za kutowsilishwa kwa taarifa hizo yalionekana kwenye mawasiliano yaliyofanyika kutoka Manispaa ya Dodoma ambapo matokeo ya ukaguzi uliofanyika kwenye kampuni za Huacheng Intrnational Ltd na S&Y Gourment Meat Co. Ltd ambapo taarifa yake haikuwasilishwa kwa wadau kama vile Mamlaka ya Chakula na Dawa, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Afya, Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wala Ofisi ya RAS-Dodoma. Matokeo ya taarifa hii ykuwasilishwa katika Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ni kuchukua hatua stahiki za kuyafungia machinjio hayo yaliyokuwa yakiendeshwa na kampuni hizo.

Katika Ukaguzi wa Usimamizi wa Mchakato wa Tathmini ya Athari za Mazingira, ilibainika kuwa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lilitakiwa kufanya mapitio ya tathmini ya athari za mazingira na hadidu za rejea kwa kipindi cha siku kumi nanne (14) baada ya siku ya kupokelewa[14]. Hata hivyo, mapitio ya miradi iliyokaguliwa yalibainisha kuwa zaidi ya nusu ya miradi (kama asilimia 53) ilicheleweshwa kufanyiwa mapitio na kutoa mrejesho kwa wamiliki wa miradi husika. Ilibainika pia kuwa asilimia 15 ya taarifa zilifanyiwa mapitio kwa wakati na taarifa kutolewa kwa wakati; na kwa asilimia 31 ya miradi, taarifa zake hazikuweza kupatikana wala kutolewa na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira .

Kwa upande mwingine, Ukaguzi wa Usimamizi wa Mikataba ya Ujenzi wa Miradi ya Maji Mijini, wahusika wa mikataba hawakutoa taarifa kwa wakati kuhusu melekezo bayana yaliyokuwa yakitolewa kutoka kwa mkandarasi au mmiliki wa mradi (Wizara ya Maji). Kwa mfano, Wizara ya Maji ilitoa malekezo ya mdomo wakati ikitoa kibali cha ongezeko la muda kwa muda wa miaka 2[15] (kuanzia 11 Machi 2012 hadi Agosti 2014) kwa mkandarasi wa mradi wa Chalinze fungu la 5. Hii ni kinyume cha kifungu 6.1 cha vifungu vya masharti ya jumla kwenye mkataba ambacho kilisisitiza kuwa mawasiliano kati ya mkandarasi na mwenye mradi yanapaswa kuwa katika maandishi. Kwa mujibu wa taarifa za maendeleo ya mradi ya Septemba 2014, haikufahamika endapo mkandarasi aliomba ongezeko hilo la muda kwani kazi zilikuwa zikiendelea. Kwa kuzingatia kwamba maelekezo yoyote ya mdomo yasingeweza kuwa na nguvu kisheria endapo kutatokea mgogoro wa kimkataba, hii inaweza kusababisha gharama kwa serikali.

[14] Kanuni ya 13 (2) Kanuni za tathmini na ukaguzi wa mazingira, 2005

[15] Septemba 2014 taarifa ya maendeleo ya kila mwezi ya Fungu la 5.

Mapungufu yalibainika pia katika uratibu na ushirikishanaji wa taarifa ndani ya taasisi za serikali. Katika Ukaguzi wa Usimamizi wa Mchakato wa Tathmini ya Athari za Mazingira, ilibainika kuwepo kwa mapungufu katika kusambaza dondoo za miradi kwenye halmashauri husika. Wakaguzi walibaini kutokuwepo kwa dondoo za miradi ambazo zilifanyiwa mapitio na maofisa mazingira wa wilaya katika halmashauri zote zilizokaguliwa. Hii ilitokana na ukweli kuwa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira halikuwasilisha kikamilifu dondoo za miradi kwenye halmashauri husika kwa ajili ya mapitio na maoni. Ni asilimia 5 tu ya dondoo za miradi kwenye halmashauri zilizokaguliwa ziliwasilishwa kwenye halmashauri husika kama inavyoainishwa kwenye Jedwali 3.5 hapa chini.

**Jedwali 3.5: Uwiano wa dondoo za miradi iliyopokelewa kutoka Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na halmashauri mikoani**

| Na. | Mwaka wa fedha | Idadi ya miradi inayotekelezwa kwenye halmashauri | Idadi ya dondoo za miradi zilizopokelewa kitoka Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira |
|---|---|---|---|
| 1 | 2010/2011 | 14 | 0 |
| 2 | 2011/2012 | 17 | 0 |
| 3 | 2012/2013 | 5 | 0 |
| 4 | 2013/2014 | 11 | 0 |
| 5 | 2014/2015 | 8 | 3[16] |
| **Jumla** | | **55** | **3** |

**Chanzo: Taarifa zilizokusanywa kutoka kwenye halmashauri zilizotembelewa (Taarifa za utendaji kuhusu Usimamizi wa Mchakato wa Tathmini ya Athari za Mazingira kwenye miradi ya maendeleo)**

Jedwali 3.5 linaonesha kuwa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira halikuwapatia maofisa mazingira nafasi ya kutoa maoni juu ya miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao. Hii ni kinyume cha kanuni za tathmini ya athari za mazingira na ukaguzi.[17]

[16] Halmashauri ya jiji la Mbeya (taarifa ya miradi miwili) na Tanga (taarifa moja ya miradi) .

[17] Kanuni ya 8(1)(b) yatathmini ya athari na ukaguzi wa mazingira, 2005.

**Jedwali 3.6: Miradi yenye cheti cha tathmini ya athari za mazingira kutoka Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira bila Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuwa na taarifa**

| Mwaka wa fedha | Idadi ya miradi yenye cheti cha tathmini ya Athari za mazingira | Idadi ya miradi yenye tamko la taarifa ya tathmini ya athari za mazingirailiyowasilishwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI |
|---|---|---|
| 2010/2011 | 149 | Hakuna |
| 2011/2012 | 157 | Hakuna |
| 2012/2013 | 290 | Hakuna |
| 2013/2014 | 256 | Hakuna |
| 2014/2015 | 1098 | Hakuna |
| **Jumla** | 1950 | Hakuna |

**Chanzo: Rejesta ya miradi Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, pamoja na mahojiano na maofisa wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI**

### 3.6.3 Mrejesho kuhusiana na taarifa zilizowasilishwa

Kulikuwepo na mapungufu hasa kwa upande wa matumizi ya taarifa wakati wa kutoa mrejesho kwenye mamlaka husika. Wakati wa Ukaguzi wa mchakato wa Udhibiti wa Afya kwenye Uzalishaji wa Nyama, ilibainika kuwa kulikuwepo na mrejesho wa maandishi kwenda kwenye halmashauri kuhusiana na taarifa za maendeleo zilizowasilishwa kwenye mamalaka za juu za kisekta. Hata hivyo, kati ya sekretarieti za mikoa sita zilizotembelewa, ni Dar es Salaam na Rukwa pekee ndizo zilizofanya ufuatiliaji na tathmini ya machinjio ambayo haikujielekeza kwenye mambo ya afya kwenye mchakato wa uzalishaji wa nyama.

Mapendekezo mbalimbali yaliyotokana na ufuatiliaji na tathmini kuhusu uboreshaji wa hali ya afya kwenye machinjio yalitolewa kwenda kwenye halmashauri kwa ajili ya utekelezaji na usimamizi. Mapendekezo yaliyotolewa yalilenga kutatua changamoto mbalimbali kama vile uboreshaji wa miundombinu ya machinjio, usambazaji wa maji safi na salama, tiba stahiki, na uharibifu wa taka zitokanazo na machinjio, na usimamizi mzuri wa wanyama ikiwemo utumiaji wa vifaa vya usalama.


Halmashauri zilipeleka taarifa za kila mwezi na robo mwaka kwenda kwenye Sekretarieti za Mkoa. Halmashauri ambazo hazikupeleka taarifa hizo zilikumbushwa kufanya hivyo. Mapitio ya nyaraka hizo kwa mkoa wa Dar es Salaam yalibainisha kutokufanyika kwa uchambuzi kwenye taarifa zilizowasilishwa na hakuna mrejesho wa taarifa hizo uliopelekwa kwenye halmashauri husika. Aidha, Sekretarieti za Mkoa hazikuwasilisha kwenye wizara taarifa yoyote ya jumla iliyoonesha hali ya uzingatiaji wa mahitaji ya usafi katika mchakato wa uzalishaji wa nyama.

Kwa upande mwingine, katika Ukaguzi wa Usimamizi wa Utoaji Huduma za Ugani, ilibainika kwamba halmashauri hazikupokea mrejesho kutoka Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kutoka kwenye taarifa za maendeleo za robo mwaka na zile za mwaka ingawa kulikuwepo na mfumo mzuri wa mrejesho kuanzia ngazi ya kijiji hadi wizarani. Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa taarifa nne za mwaka[18] kutoka Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Rais -TAMISEMI na taarifa 35 za robo mwaka zilizowasilishwa kwenye Sekretarieti za Mkoa kutoka kwenye halmashauri 10 zilizokaguliwa.

Taarifa za maendeleo za mwaka pamoja na za robo mwaka zilijumuisha malengo ya Halmashauri na changamoto zinazokumbana nazo ili kufikia malengo ambayo yameainishwa. Hata hivyo, kinyume cha mahitaji ya Miongozo ya Uongozaji na Usimamizi wa Huduma za Ugani za Mwaka 2009 na Miongozo ya Ufuatiliaji na Uthamini za Mwaka 2008, ambazo zinahitaji wizara za kisekta kupokea taarifa za maendeleo za robo mwaka na za mwaka, kuzichambua kwa kina na kutoa mrejesho kwenye halmashauri kupitia Sekretarieti za Mkoa, ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa mrejesho wowote uliotolewa kwenda kwenye halmashauri juu ya taarifa zilizowasilishwa.

[18] 2009/2010, 2010/2011, 2011/2012 na 2012/2013

**Kielelezo 3.1: Uhusiano wa matokeo ya ukaguzi katika usimamizi wa taarifa kwenye sekta ya umma**



# SURA YA NNE

# UPIMAJI WA UTENDAJI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inaonesha matokeo ya jumla kutokana na kaguzi sita za ufanisi zinazohusu upimaji wa utendaji katika sekta za umma. Sura imejikita zaidi katika kuangalia uanzishaji wa mifumo ya upimaji wa utendaji wa kazi, kutambua na kuchagua viashiria vya upimaji wa utendaji, uandaaji wa mipango ya upimaji wa utendaji, kukusanya na kuchambua taarifa za utendaji, kutafsiri taarifa za utendaji, kuchukua hatua madhubuti, uandaaji, na utoaji wa mrejesho.

## 4.2 Lengo la kupima utendaji katika sekta ya umma

Lengo kuu la kupima utendaji ni kuangalia namna ambavyo shughuli zinazohusu upimaji wa utendaji katika Wizara, Idara na Wakala wa serikali unavyofanyika ipasavyo. Hasa ililenga kuangalia kwa kina:

- kiwango cha upimaji wa utendaji katika sekta za umma kama ilivyoonekana katika kaguzi zilizofanywa; na
- Iwapo taarifa za utendaji zinazowasilishwa kwa wadau zinatumika kwa maamuzi na maboresho yanafanyika ipasavyo.

Kulingana na matokeo ya kaguzi sita (6) za ufanisi katika taasisi mbalimbali za umma kuhusu upimaji wa utendaji, kuna masuala ambayo serikali inahitaji kuyasimamia ili kuleta tija na ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Maeneo hayo yana uhusiano mkubwa na yanaathiri ufanisi wa kila mmoja. Maeneo hayo ni kama ilivyo hapa chini.

## 4.3 Kukosekana kwa tathmini ya matokeo ya utendaji kwa kuzingatia malengo

Matokeo ya kaguzi sita (6) za ufanisi zilizofanywa zinaonesha kuwa uwepo wa matatizo katika utoaji wa huduma unahusishwa na udhaifu katika upimaji wa utendaji. Jedwali 4.1 linaonesha tathmini ya upimaji wa ufanisi kama ilivyochambuliwa na wakaguzi.

**Jedwali 4.1: Tathmini ya upimaji wa utendaji kwa taasisi za umma**

| Suala la kiutendaji | Taasisi | Upimaji wa utendaji | |
|---|---|---|---|
| | | Taarifa zinazohusu fedha | Taarifa zisizohusu fedha |
| Ubora wa Elimu | Wizara ya Elimu | Ndio | Ndio[19] |
| | Ofisi ya Rais-TAMISEMI | Ndio | Ndio[20] |
| Utoaji wa Huduma za Ugani | Ofisi ya Rais-TAMISEMI | Ndio | Ndio[21] |
| | Wizara ya Kilimo | Ndio | Ndio[22] |
| Udhibiti wa Usafi kwenye Uzalisha wa Nyama | Wizara ya Afya | Ndio | Hapana |
| | Ofisi ya Rais-TAMISEMI | Ndio | Hapana |
| | Wizara ya Kilimo | Ndio | Hapana |
| Udhibiti wa Magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea | Ofisi ya Rais-TAMISEMI | Ndio | Hapana |
| | Wizara ya Kilimo | Ndio | Hapana |
| Usimamizi wa Mikataba | Wizara ya Maji | Ndio | Ndio |
| Uthibiti wa Athari za Mazingira | Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira | Ndio | Hapana |
| | Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira | Ndio | Hapana |

**Chanzo: Tathmini ya wakaguzi**

---

19 Ubora wa elimu unapimwa kwa kuangalia matokeo yanayotelewa na baraza la taifa la mitihani.

20 Ubora wa elimu unapimwa kwa kuangalia matokeo yanayotelewa na baraza la taifa la mitihani.

21 Hata hivyo, taarifa za Utendaji kwa shughuli amabazo hazikuwapo katika program ya maendeleo ya sekta ya Kilimo hazikupatikana.

22 Hata hivyo, taarifa za Utendaji kwa shughuli amabazo hazikuwapo katika program ya maendeleo ya sekta ya Kilimo hazikupatikana.

Jedwali 4.1 linaonesha kuwa taasisi zilizokaguliwa zinafanya tathmini ya utendaji wao. Hata hivyo tathmini ilijikita zaidi katika kutathmini matumizi ya fedha kwa sababu zinatakiwa kuandaa taarifa ya fedha kwa ajili ya ukaguzi. Iligundulika kuwa taasisi zilizokaguliwa zilikuwa zinatumia mipango mkakati na mipango ya kati ya matumizi katika kupima utendaji wao. Taarifa ya mwaka ya utekelezaji ilikuwa inaandaliwa kwa kuangalia fedha zilizopangwa, zilizotumika, na zisizotumika na shughuli zilizofanywa kwa mwaka huo.

Iligundulika kuwa katika taarifa sita (6) za kaguzi za ufanisi kulikuwa na mapungufu kwenye mfumo wa upimaji wa utendaji katika sekta za umma. Hali hiyo imesababisha uwepo wa huduma zisizoridhisha kwenye taasisi zilizokaguliwa na kusababisha utoaji hafifu wa huduma kwa wananchi. Hali ya kutoa huduma hafifu inatokana na wizara na taasisi husika kutokuwa na taarifa juu ya matatizo ya kiutendaji katika sekta hizo.

Jedwali 4.2 linaonesha baadhi ya mifano itokanayo na athari ya taasisi husika kushindwa kuelewa hali ya utendaji wake wa kazi. Mifano hiyo ni kutoka kwenye ripoti sita za ukaguzi.

**Jedwali 4.2: Athari za kutokuwa na mfumo thabiti wa upimaji wa utendaji katika utoaji wa huduma kwa taasisi zilizokaguliwa**

| Taarifa ya Ukaguzi wa ufanisi | Mandhara |
|---|---|
| Utoaji wa Huduma za Ugani | Halmashauri nyingi zilizotembelewa zina tatizo la njaa kipindi cha kiangazi. Uzalishaji mdogo unatokana na wananchi kutokutumia njia bora za kilimo katika mashamba yao. |
| Usimamizi wa Magonjwa na Wadudu Waharibifu wa mimea | Heka zilizoharibiwa ziliongezeka kutoka 591 hadi 1344 kwa mwaka 2013-2014; na migomba iliyong'olewa ilikuwa asilimia 84 kwa miezi minne kuanzia mwezi wa sita hadi wa tisa, 2015. |
| Ubora wa Huduma za Elimu | Inasababisha kuwa na utendaji usioridhisha kwa walimu na utekelezaji hafifu wa mitaala na kusababisha wanafunzi wengi kufanya vibaya katika masomo yao. |
| Udhibiti wa Uchafu kwenye Uzalishaji wa Nyama | Asilimia 75 ya machinjio kumi na mbili (12) yaliyotembelewa yanafanya kazi katika mazingira yanayohatarisha afya ya walaji wa nyama. |
| Mchakato wa Tathmini za Athari za Mazingira | Miradi 3,811 kati ya 15,266 iliyosajiliwa na bodi ya usajili ya makandarasi haikusajiliwa na Baraza la Hifadhi na na Usimamizi wa Mazingira. |
| Usimamizi wa Mikataba katika Ujenzi wa Miradi ya Maji Mijini | Pamoja na kuonesha kuwa kazi ilifanyika kwa kiwango cha chini kwa sehemu ya mkataba F & H hadi kusababibisha kuvunjwa kwa mkataba, kiwango cha malipo ya fedha cha Shilingi bilioni 7.5 kilikuwa kimeidhinishwa na mshauri na kulipwa na Wizara. |

**Chanzo: Sehemu ya Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi, 2015[23] & 2016[24]**

Jedwali 4.2 linaonesha kuwa katika taarifa sita za kaguzi za ufanisi zinaonesha mapungufu katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

[23] Utoaji wa Huduma za Ugani.

[24] Usimamizi wa Mgonjwa na Wadudu Waharibifu wa Mimea, Ubora wa Huduma za Elimu, Udhibiti wa Uchafu kwenye Uzalishaji wa Nyama, Usimamizi wa Mikataba katika Ujenzi wa Miradi ya Maji Mijini na Mchakato wa tathmini za athati za mazingira.

Mapungufu hayo yalitokana na kushindwa kufikia malengo yaliyopangwa, kucheleweshа utoaji wa huduma, huduma zitolewazo kutoridhisha, na gharama za utekelezaji wa huduma kuzidi zilizopangwa. Uchambuzi uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu inaonesha kuwa hali hii inatokana na kukosekana kwa mfumo wa kupima utendaji katika utoaji wa huduma katika taasisi za umma.

Ilionekana kuwa mfumo wa upimaji wa utendaji ulikuwa kwa miradi au programu zinazofadhiliwa na washirika wa maendeleo, ambapo moja ya kigezo ni kuwa na mfumo wa upimaji wa utendaji kwenye miradi au programu hizo. Hii inaonesha kuwa taasisi za umma hazioni umuhimu wa kupima utendaji kwenye utoaji wa huduma zinazofadhiliwa na fedha za ndani.

Vilevile iligundulika kuwa upimaji wa utendaji unafanywa hasa kwa kuangalia ufanisi wa fedha kwa kulinganisha fedha zilizotengwa na zilizotumika. Taarifa za mwaka zilizoandaliwa na taasisi zilizokaguliwa zinaonesha kuwa taasisi hizo zinajikita zaidi katika kuonesha kiwango cha fedha ambazo hazikupata kuliko kiwango cha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na malengo waliyojiwekea.

## 4.4 Mkazo finyu kwenye viasharia vya utendaji ambavyo si vya upimaji wa fedha

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu imeona kuwa uanishaji na uchambazi wa viashiria vya upimaji wa utendaji katika sekta za umma kwenye utoaji wa huduma au utekelezaji wa miradi ya maendeleo haufanyiki ipasavyo. Hii iligundulika kwenye ripoti tatu (3) kati ya sita (6) za ukaguzi wa ufanisi[1] zilizojumuishwa katika ripoti hii.

[25]

Ripoti hizo tatu za ukaguzi zilionesha kuwa taasisi saba (7) zilizokaguliwa hazikuwa na viashiria vya kupima utoaji wa huduma kwa wananchi hivyo kusababisha kutoa taarifa ya ufanisi wa fedha na kuachana na taarifa zinazohusu ubora na utoaji wa huduma kwa wakati.

[25]Usimamizi wa Majonjwa na Wadudu Waharibifu wa Mimea, Udhibiti wa Uchafu kwenye Uzalishaji wa Nyama, na Mchakato wa Tathmini za Athari za Mazingira

**Kielelezo 4.1. Uhusiano kati ya programu au malengo na viashiria vya upimaji wa utendaji**

| Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi | Malengo | Matokeo ya Ukaguzi ambayo yangeweza kuzuiliwa kama kungekuwa na viashiria vizuri vya kupimaji utendaji |
|---|---|---|
| Utoaji wa Huduma za Ugani | Kuongeza uzalishaji kwa wakulima wadogo wadogo kwa kuwawezesha kutumia teknolojia ya kisasa kwa kuimarisha huduma za ugani kwa wakulima | Wakulima wachache walifundishwa njia bora za kilimo, mashamba ya mfano na mashamba darasa hayakuanzishwa ipasavyo vijijini na wakulima wengi bado wanatumia njia ya zamani |
| Usimamizi wa Magonjwa na Wadudu Waharibifu wa Mimea | Kuongeza uzalishaji kwa kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea | Kuna milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea karibu kila mkoa, uchunguzi wa kina haufanyiki mara kwa mara kwa magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea na utekelezaji hafifu wa kutabiri uwezekano wa milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea |
| Ubora wa Huduma za Elimu | Kuimarisha ubora wa elimu ya msingi na sekondari kwa kuongeza hali ya ufaulu kwa kuimarisha ufundishaji, upatikanaji wa zana za kujifunzia na kufundishia na kusimamia ufanisi wa walimu. | Kuna uwepo wa walimu wasio na sifa, mgawanyo usio sawa wa walimu, upungufu wa vitabu na upungufu katika usambazaji wa taarifa za uchambuzi wa mitihani |
| Udhibiti wa Usafi kwenye Uzalishaji wa Nyama | Kulinda afya na usalama wa wananchi kwa kuhakikisha kuna udhibiti wa usafi katika uzalishaji wa nyama. | Asilimia 75 ya machinjio yanaendeshwa katika mazingira ya uchafu, kuna machinjio yanayofanya kazi ambayo hayajasajiliwa, na kuna baadhi ya magari yanayotumika kusafirishia nyama ambayo hayajakidhi vigezo vya usafi. |

| Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi | Malengo | Matokeo ya Ukaguzi ambayo yangeweza kuzuiliwa kama kungekuwa na viashiria vizuri vya kupimaji utendaji |
|---|---|---|
| Mchakato wa Tathmini za Athari za Mazingira | Kuhakikisha kuwa miradi yote ambayo ina athari inasajiliwa, tathminiwa na kuchukua hatua za kupunguza athari kama inavyooneshwa kwenye Taarifa ya Tathmini ya Athari za Mazingira. | Mchakato unaotumiwa na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira katika kuchukua miradi ya kufanyia tathmini unategemea uaminifu kwa anayeendeleza mradi na inashindwa kutambua baadhi ya vitu venye athari ya kimazingira, kama ilivyo kuwa ujenzi wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi |
| Usimamizi wa Mikataba katika Ujenzi wa Miradi ya Maji Mijini | Kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa Watanzania kwa njia ya utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya maji mijini | Kuna ubora hafifu kwenye miradi ya ujenzi wa maji, miradi haimaliziki kwa wakati, na kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi |

**Chanzo: Sehemu ya taarifa ya ukaguzi za ufanisi, 2015[26] & 2016[27]**

Kielelezo 4.1 kinaonesha kuwa ugunduzi na uchambuzi wa viashiria vya ufanisi vinavyotumiwa na taasisi zilizokaguliwa haujumuishi baadhi ya vitu vinavyochangia mafanikio ya malengo kwa ujumla.

Kwa mfano, kwenye Ukaguzi wa Ufanisi uliohusu Utoaji wa Huduma za Ugani iligundulika kuwa programu ya maendeleo ya kilimo haikujumuisha masuala yanayohusu upatikanaji wa soko. Hii inazuia maana ya kuongeza faida na mapato kwa wakulima.

[26] Utoaji wa Huduma za Ugani.

[27] Usimamizi wa Magonnjwa na Wadudu Waharibifu wa Mimea, Ubora wa huduma za Elimu, Udhibiti wa Uchafu kwenye Uzalishaji wa Nyama, Usimamizi wa Mikataba katika Ujenzi wa Miradi ya Maji Mijini na Mchakato wa Tathmini za Athari za Mazingira.

Pia iligundulika kwenye Ukaguzi wa Ufanisi wa Mchakato wa Tathmini za Athari za Mazingira kuwa njia zilizokuwa zinatumiwa na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kutambua miradi zilitegemea zaidi uaminifu kwa mtu anayeendeleza miradi na zimeshindwa kutambua baadhi ya masuala yenye athari za kimazingira. Hali hiyo ilisababisha baadhi ya miradi yenye athari kimazingira kutotambuliwa na kusajiliwa na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Baadhi ya miradi ilisajiliwa bila ya kujali njia za kuzuia athari za kimazingira kwa miradi iliyopo kwenye maeneo hatarishi kama vile kwenye maeneo ya majimaji ambayo ni muhimu kuruhusu maji kupita kwa urahisi.

Kadhalika, kwenye Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Mikataba kwenye Miradi ya Ujenzi ya Maji Mjini iligundulika kuwa miradi hiyo ilikuwa na matatizo yaliyosababishwa na usanifu mbaya wa miradi uliosababisha ongezeko la gharama, kuchelewa kukamilika kwa miradi, na kushindwa kutambua masuala muhimu katika usimamizi wa miradi. Uchambuzi hafifu wa viashiria vya ufanisi vinasababisha yafuatayo:

i. ***Kuongezeka kwa gharama za ujenzi wa miradi ya maji iliyokaguliwa kwa shilingi bilioni 3.015 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 4.3***

**Jedwali 4.3: Ongezeko la gharama kutokana na mapungufu katika kuangalia ufanisi wa mradi**

| Vitu vilivyoongezeka | Gharama yake (Sh. Milioni) |
|---|---|
| Bomba la maji la kilomita 70 kuongezewa | 2,220 |
| Alama zinazoonesha kuwepo kwa bomba la maji | 23 |
| Utafiti wa kuonesha muonekano wa eneo husika | 77 |
| Kuonyesha eneo la kuvukia waenda kwa miguu na eneo ambalo mto unakatisha | 682 |
| Vijiji vinne havikuwepo kwenye mchoro wa awali | 13[28] |
| **Jumla** | **3,015** |

**Chanzo: Taarifa ya ukaguzi wa ufanisi kwenye usimamizi wa miradi ya maji mijini, 2016.**

[28] Awali ilikuwa kwa Dola za Marekani 6,000 ambayo ni sawa na Shilingi 13, 200,000

### *ii Kutokukamilika kwa miradi kwa wakati*

Pia Ukaguzi wa Usimamizi wa Mkataba katika Miradi ya Maji Mijini iligundulika kuchelewa kwa kukamilika miradi kuanzia miezi tisa (9) hadi miaka mine (4), kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 4.4 hapo chini. Baadhi ya sababu zilizosababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi ni kuwa baadhi ya vitu havikuweka kwenye makadilio ya awali ya gharama ya ujenzi.

**Jedwali 4.4: Tofauti kati ya muda uliopangwa na muda uliotumika mpaka kukamilika kwa kazi**

| Number ya mkataba | Muda uliopangwa (Miezi) | Muda ulioongezwa (Miezi) | Asilimia ya muda ulioongezwa | Hali ya kazi ilipofika |
|---|---|---|---|---|
| Mradi wa Chalinze kipande 1 | 18 | 9.5 | 53 | Umekamilika |
| Mradi wa Chalinze Kipande 2 | 17 | 23 | 135 | Uko kwenye hatua za mwisho |
| Mradi wa Chalinze Kipande 3 | 17 | 35 | 206 | unaendelea |
| Mradi wa Chalinze Kipande 5 | 18 | 45 | 250 | Uko kwenye hatua za mwisho |
| Mradi wa Chalinze Kipande 6 | 18 | 40.5 | 225 | Uko kwenye hatua za mwisho |
| Mradi wa Bukoba | 18 | 14 | 78 | unaendelea |
| Mradi wa Musoma | 18 | 12 | 67 | unaendelea |
| Mradi wa Chalinze Kipande F & H - kazi zilizobaki | 9 | 9 | 100 | unaendelea |

**Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi wa ufanisi kwenye Usimamizi wa Miradi ya Maji Mijini, 2016.**

Jedwali 4.4 linaonesha kuwa miradi ya ujenzi wa maji haikukamilika kwa muda uliopangwa. Hii ni kutokana na ongezeko la muda ambalo ni mara 2.5 ya muda uliyopangwa.

Ongezeko la muda linatokana na: (1) Makandarasi kutokuwa na watu muhimu kwenye eneo la mradi wa kuweza kusimamia ujenzi (2) kuchelewa kwa malipo ya awali na malipo ya kazi inayoendelea kutokana na matatizo ya fedha serikalini (3) kasi ndogo ya makandarasi kutokana na wafanyakazi wachache na kukosekana vifaa vya ujenzi (4) kucheleweshwa kuidhinisha mabadiliko yaliyofanywa kwenye aina ya bomba la maji (5) kuongezeka kwa kazi iliyotakiwa kufanyika kwa mujibu wa mkataba.

Kwa upande mwingine, yafuatayo yaligundulika kwenye Taarifa ya Ukaguzi wa Mchakato wa Tathmini za Athari za Mazingira:

### *iii Taarifa za ufanisi hazichambuliwi ipasavyo*

Taarifa ya Ukaguzi wa Mchakato wa Tathmini za Athari za Mazingira inaonesha kuwapo kwa tofauti kubwa kati ya taarifa zilizopangwa kupitiwa na zilizopitiwa na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Taarifa za miradi iliyopitiwa zinazidi zilizopangwa kwa asilimia kati ya 241-722 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 4.5

**Jedwali 4.5: Idadi ya miradi iliyopangwa na iliyopitiwa na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

| Mwaka wa fedha | Idadi ya miradi iliyopangwa kupitiwa | Idadi ya miradi iliyopitiwa na iliyosajiliwa | (%)asilimia iliyozidi |
|---|---|---|---|
| 2010/11 | 50 | 411 | 722 |
| 2011/12 | 100 | 481 | 381 |
| 2012/13 | 150 | 749 | 599 |
| 2013/14 | 100 | 463 | 563 |
| 2014/15 | 500 | 1,707 | 241 |

**Chanzo: Regista na mipango ya mwaka 2010/11-2014/15 ya Baraza la Hifadhi na na Usimamizi wa Mazingira**

Jedwali 4.5 linaonesha kuwa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira halijifunzi kutokana na utendaji wa miaka inayopita ili kuweza kuboresha utendaji wa mwaka unaofuata. Kwa mfano, mwaka 2010/11 hadi 2012/13 lilipanga kuangalia miradi 150 ambayo ilikuwa ni idadi ndogo kuliko ya mwaka uliofuata ya kuangalia miradi 100. Ingawa kiwango kilichopangwa cha utendaji kilipanda hadi kufikia miradi 500, idadi ya taarifa za miradi zilizopitiwa zilikuwa zinapanda. Hii inaonesha kuna mapungufu katika kutambua na kuchagua viashiria vya kupima utendaji wa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kuhusu tathmini ya athari za kimazingira.

### *iv Kushindwa kuzingatia masuala muhimu kwenye tathmini za athari za kimazingira kwenye Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi ya Dar es salaam*

Tathmini ya athari za mazingira kwa Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi inaonesha kuwa baadhi ya masuala muhimu yenye athari za mazingira hayakuangaliwa. Kwa mfano, suala la Mto Msimbazi halikuangaliwa wakati wa ujenzi wa kituo cha mabasi cha Jangwani. Vilevile taarifa haikuainisha njia za kupunguza athari za mazingira kwenye ujenzi wa kituo hicho kikubwa cha mabasi yaendayo kasi. Hali hii inasabibisha uwepo wa mafuriko kwenye eneo hilo kwani maji yamekuwa yakijaa na kusambaa kwenye kituo cha mabasi na kwenye makazi ya watu.

Pia, tathmini hiyo ya athari za mazingira haikuzingatia suala la usimamizi wa maafa kwani haikujenga barabara ndogo ya kuwezesha kuingi na kutoka kwenye ofisi za kuzalishia umeme zilizopo Ubungo. Hali hii inapelekea usumbufu wakati wa kuingia katika ofisi hizo.

## 4.5 Hakuna uhusiano kati ya viashiria vya ufanisi/ utendaji na malengo ya juu ya taasisi

Uchambuzi wa malengo kwa taasisi zilizokaguliwa unaonesha kuwepo kwa mapungufu kwenye mahusiano kati ya viashiria vya utendaji na malengo makuu ya taasisi kama inavyoelezwa hapa chini.

Kwenye Ukaguzi wa Ufanisi wa Udhibiti Uchafu kwenye Maeneo ya Uzalishaji wa Nyama inaonesha kuwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi; na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hazikuwa na viashiria vya kupima utendaji kwenye masuala ya udhibiti wa usafi kwenye uzalishaji wa nyama.

Vilevile, iligundulika kwenye Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Tathmini ya Athari za Mazingira kuwa Ofisi ya Makamu Rais haina viashiria vya kupima utendaji wa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira katika shughuli za kusimamia tathmini ya athari za mazingira kwa miradi husika.

Shughuli za kutathmini athari za mazingira ilibainika kuwa kulikosekana viashiria vya kupima utendaji kwenye idadi ya miradi iliyosajiliwa na Baraza la Hifadhi na na Usimamizi wa Mazingira. Pia, kulibainika kutolewa kwa vibali vya ujenzi bila ya kufanyika kwa tathmini ya athari za mazingira na kuchambua miradi ya maendeleo inayotakiwa kufanyiwa tathmini ya athari za mazingira.

Kwa upande mwingine, Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kwenye Huduma za Ugani, inaonesha kuwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI; na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi zimeandaa viashiria vya kupima utendaji wa maofisa ugani kwa ngazi ya kata na kijiji, maofisa wa kilimo wa wilaya, tawala za mikoa, na Ofisi za kilimo za kanda. Viashiria vilivyoandaliwa vilikuwa vinajumuisha huduma za ugani na upimaji wa ufanisi katika upimaji na matokeo ya programu ya maendeleo ya sekta ya kilimo.

Hata hivyo, ukaguzi wa ufanisi kwenye usimamizi wa milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea nchini iligundulika kuwa wizara hizo za Ofisi ya Rais - TAMISEMI ,Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi zilikuwa na viashiaria vya kupima ufanisi katika eneo hili la milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea, lakini viashiria hivyo havikuweza kuonesha matokeo halisi ya kupata utekelezaji wa mipango hiyo ya kukabiliana na milipuko husika. Hii inaonyesha kuwa wizara zimeshindwa kuwa na viashiria vya utendaji vinavyopima matokeo halisi ya shughuli za kudhibiti milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea.

Vilevile, kwenye eneo hilohilo la milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea, imegundulika kuwa hapakuwa na viashiria vya kupima ufanisi wa watendaji waliopo kwenye Ofisi za Tawala za Mikoa, Ofisi za kanda na zile za serikali za mitaa katika kudhibiti milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu.

Katika taarifa mbili za ukaguzi wa ufanisi[29], viashiria vya utendaji vilijikita katika kuangalia malengo kwa shughuli zilizopangwa kufanyika. Viashiria hivyo vilivyowekwa vilishindwa kuonesha hali halisi ya utekelezaji wa malengo husika.

Kwenye Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Magonjwa na Wadudu Waharibifu wa Mimea iligundulika kuwa viashiria vya kupima utendaji katika usimamizi wa shughuli za kudhibiti milipuko hivyo havikuangalia masuala yote muhimu.

Ripoti za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Kilimo kwa wilaya zote saba (7) zilizotembelewa[30] zimeonyesha kuwa masuala yanayohusu usimamizi wa magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea hayakujumuishwa kwenye shughuli za ufuatiliaji katika wilaya husika. Kipengele pekee kilichokuwa kinajumuishwa ni mafunzo yaliyokuwa yanatolewa kwa wakulima japo nayo hayakuwa yakifanyika kikamilifu.

[29] Ubora wa elimu na usimamizi wa Magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea
[30] Halmashauri hizo ni ya Muleba, Meru, Bahi, Nanyumbu, Mbarali, Masasi and Lushoto

Vilevile, kwenye Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi katika Ubora wa Elimu kwa shule za msingi na sekondari iligundulika kuwa viashiria vya kupima ufanisi zilijikita kwenye malengo na madhumuni ya kutekeleza shughuli zilizopangwa. Hata hivyo, hapakuwapo na malengo halisi ya utendaji. Iiligundulika kuwa kwa kukosa malengo halisi ya utendaji, ilikuwa vigumu sana kupima utendaji katika kuboresha ubora wa elimu.

Wakati wa ukaguzi wa eneo hilohilo la utoaji wa elimu bora kwa shule za msingi na sekondari, iligundulika kuwa mfumo wa upimaji wa utendaji kwa njia ya mfumo wa wazi wa kupima utendaji haukuwa unafaa kupima utendaji wa walimu kwa kuwa mfumo huo hauna viashiria vinavyoendana na mazingira ya walimu. Iligundulika kuwa tathmini hizo hazikuwa zinazingatia mchango wa mwalimu katika ufaulu wa mwanafunzi.

Iligundulika kuwa kukosekana kwa viashiria vya utendaji kunazuia taasisi za umma kuangalia kiwango na ubora wa huduma zinazotoa kwa wananchi kwa maeneo mbalimbali kama vile huduma ya elimu bora, usimamizi wa udhibiti wa usafi, usimamizi wa magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea na usimamizi wa mchakato wa kutathmini athari ya mazingira kwa miradi mbalimbali nchini. Hali hii inahatarisha uwezekano wa serikali kutoa huduma kwa wananchi ipasavyo.

Iligundulika kuwa hali hii inazuia uwajibikaji kwa sababu ni vigumu kwa wizara kupima utendaji wa taasisi zinazowajibika kwake. Kwa hivyo, ni vigumu kwa wizara kuchukua uamuzi sahihi kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma. Mifano ya maeneo yanayohitaji kufanyiwa maboresho ni kama ilivyoonyeshwa kwenye **Jedwali 3.2.**

Kutokana na kushindwa kutambua, kuchambua, na kuweka viashiria vya kupima utendaji katika sekta za umma, taasisi kumi na moja (11) zilizokaguliwa isipokuwa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknologia na Mafunzo ya Ufundi zilishindwa kuchukua uamuzi wa kuimarisha viashiria vya kupima utendaji wa watumishi wake.

Kwa mfano, kwenye Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Ubora wa Elimu inaonesha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi; Ofisi ya Rais – TAMISEMI; na Chama cha Walimu Tanzania kimeamua kurekebisha Mfumo wa Wazi wa Kupima Ufanisi wa walimu usioendana na mazingira ya kufundisha na kuweka hali halisi ya ufanisi wa walimu.

Kwa maeneo mengine ya utoaji wa huduma za ugani; usimamizi wa magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea, udhibiti wa usafi kwenye uzalishaji wa nyama; na tathmini athari za mazingira kwenye miradi ya maendeleo hakuchukuliwa hatua za kuimarisha viashiria vya utendaji katika maeneo hayo.

### 4.6 Kutokuandaa mipango ya upimaji wa utendaji

Kaguzi zote sita za ufanisi zinaonesha kuwa hapakuwa na taasisi yeyote ile iliyoandaa mpango wa kupima utendaji wa shughuli zao na za taasisi zinazozisimamia katika utoaji wa huduma husika.

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Uboreshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari inaonesha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia, na Mafunzo ya Ufundi kupitia Idara ya Ukaguzi haikuweza kukagua shule zote ndani ya miaka miwili kama inavyooneshwa kwenye Muongozo wa Ukaguzi wa Shule wa Mwaka 2010. Vilevile kuna shule ambazo hazijakaguliwa kwa kipindi cha miaka mitano mpaka kumi tofauti na shule za binafsi ambazo zilikuwa zinakaguliwa mara kwa mara kwa sababu zinalipa ada ya ukaguzi.


Ukaguzi wa Usimamizi wa Magonjwa na Wadudu Waharibifu wa Mimea unaonesha kuwa pamoja na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupanga kufanya ufuatiliaji kwenye shughuli za kilimo kwa halmashauri zake, shughuli zinazohusu milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea hazikuweza kufuatiliwa kwani nguvu kubwa iliwekwa kwenye kufuatilia na kisimamia shughuli zilizokuwa zinazohusu Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ambapo masuala yahusuyo magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea hayakuguswa.

Kwa kuongezea, Ukaguzi wa Ufanisi kwenye Usimamizi wa Mikataba kwenye Sekta ya Maji ilionesha kuwa mshauri alitakiwa aandae taarifa ya maendeleo ya ujenzi kwa kila mwezi na kutuma Wizara ya Maji na Umwagiliaji, lakini iligundulika kuwa taarifa za maendeleo za mwezi zilikuwa haziandaliwi na kutumwa kama ilivyokuwa inatakiwa.

Kwa upande mwingine, mikutano ya mwezi ilikuwa haifanyiki mara kwa mara. Kwa kuangalia taarifa za mwezi, iligundulika kuwa mikutano ya kwenye eneo la kazi ilikuwa haifanyiki kama ilivyokuwa inatakiwa. Matokeo yake ni kuwa taasisi zilizokaguliwa zilikuwa zinafanya maamuzi ya kupima ufanisi baada ya matatizo au malamiko kutokea kwenye utoaji huduma ilikutatua hali hiyo.

Ukaguzi wa Ufanisi wa Udhibiti wa Usafi kwenye Uzalishaji wa Nyama, ulibainisha kuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilijumuisha masuala ya udhibiti wa usafi kwenye mpango wa kati wa matumizi na ilikuwa inafanya mashindano ya kitaifa ya usafi wa mazingira, ambapo usafi wa machinjio ulikuwa unatazamwa pia. Hata hivyo ilibainika kuwa hapakuwa na taarifa yeyote iliyoandaliwa na Wizara kuhusu ufanisi wa mashindano hayo kwenye udhibiti wa usafi kwenye maeneo ya uzalishaji wa nyama.

**Kielelezo 4.3: Uhusiano wa Matokeo ya Ukaguzi Katika Upimaji wa Utndaji katika Sekta ya Umma**



# SURA YA TANO

# UFUATILIAJI KATIKA SEKTA YA UMMA

## 5.1 Utangulizi

Ufuatiliaji wa Ufanisi katika shughuli za utekelezaji unawezesha kufikia malengo ya taasisi. Ufuatiliaji wa shughuli unaweza kufanywa kwa njia ya ufuatiliaji, tathmini, na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wake. Taasisi za serikali zinatakiwa kuwa na utaratibu wa wazi na unaoeleweka wa kufuatilia na kutathmini na vilevile kuwasilisha taarifa za matokeo ya utendaji kwa wadau (walengwa).

Kutokana na yaliyoonekana kwenye Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi, kuna masuala yaliyohusishwa na udhaifu wa taasisi za serikali katika kusimamia, kutathmini, na kuwasilisha taarifa za shughuli zinazohitajika ilikuhakikisha inaendesha na kusimamia shughuli zake kwa ufanisi.

Mipango hafifu huathiri utendaji mzima wa shughuli kama bajeti, usimamizi, tathmini, na utekelezaji. Tathmini hafifu inaleta mwanya wa kukosekana maboresho kwa siku za baadae kwakuwa watoa maamuzi hawapewi taarifa stahiki.

Kuna matukio yanayoonyesha kwamba upo mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na mawasiliano lakini haufanyi kazi kwa ufanisi.

## 5.2 Lengo la kuchunguza ufuatiliaji katika sekta ya umma

Lengo kuu la sehemu hii ni kuchunguza kiwango cha masuala yaliyobainika katika ukaguzi uliofanywa (kama zilivyoripotiwa katika taarifa juu ya shughuli za Wizara mbalimbali, idara na mashirika ya serikali katika utoaji wa huduma) yalivyohusishwa na udhaifu wa namna taasisi za serikali zinavyofuatilia utekelezaji wa shughuli zake. Lengo hasa la uchunguzi ni:

- Kuangalia ni kwa kiasi gani udhaifu katika usimamizi, tathmini na mawasiliano (kama sehemu ya utaratibu wa ufuatiliaji) umechangia mapungufu kama yalivyoonekana kwenye matokeo ya ukaguzi;

- Kuangalia nini kifanyike ili kuboresha hali kwa kutoa mapendekezo.

Kulingana na matokeo ya uchunguzi yaliyoshabihiana kwenye ufuatiliaji na tathmini kama zilivyoonekana katika ripoti sita (6) za ukaguzi wa ufanisi wa taasisi mbalimbali, kuna masuala yanayohitaji ufuatiliaji wa karibu wa serikali ili kuhakikisha kuwa serikali inajiendesha na kusimamia shughuli zake kwa ufanisi. Ufanisi katika shughuli za serikali ni vigumu kuonekana kutokana na udhaifu mkubwa ulioonekana zaidi katika kaguzi zilizofanyika. Maeneo yote yaliyoainishwa yameonekana kuwa na uhusiano unaoathiri kila mmoja.

## 5.3 Ufuatiliaji kwenye Utendaji wa Sekta ya Umma

Mfumo wa ufuatiliaji hutumika kama zana ya kufuatilia utekelezaji wa kazi fulani. Ufuatiliaji unaweza ukafafanuliwa kama mkusanyiko wa taratibu zinazoongoza utoaji wa taarifa kwa taasisi kwa ngazi tofauti na mbalimbali ili kusaidia kufanya maamuzi na kujifunza. Mashirika mengi kwa utartibu maalumu au usio maalumu huandaa na kutumia mfumo wa taarifa kwa malengo ya ufuatiliaji. Kwa kutumia kazi za ufuatiliaji, shirika huweza kuendelea kufuatilia maendeleo ya kufanyika kwa kazi fulani. Katika hali ya kutokuwepo kwa mfumo madhubuti wa ufuatiliaji, ingekuwa ngumu kujua kama matokeo yaliyolengwa yanafikiwa kama ilivyopangwa.

Hata hivyo, katika ukaguzi uliofanywa, imebainika kwamba shughuli za serikali hufuatiliwa kwa kiwango kisichotosheleza. Kuna udhaifu uliobainishwa katika usimamizi wa mfumo wa taarifa ili kuwezesha ufuatiliaji wa ufanisi wa taarifa uliothibitishwa wa taarifa za ubora na kiasi na tafsiri yake katika usimamizi wa taarifa muhimu. Udhaifu ulioonekana katika ufuatiliaji huashiria usimamizi dhaifu katika shughuli za sekta ya umma. Maeneo yaliyobainika kuwa na udhaifu yanahusiana na hivyo kuathiriana. Hii imesababisha kukosekana kwa ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Ukaguzi wa Mfumo wa Udhibiti wa Ubora wa Elimu umebaini baadhi ya mapungufu yanayotokana na ufuatiliaji hafifu. Kwa mfano, kukosekana kwa mpango wa uendelezaji kitaaluma wa walimu ni moja ya sababu ya kuwepo kwa walimu wasiokuwa na ujuzi, sifa, na vigezo vinavyohitajika. Hii ilisababishwa na ukosefu wa chombo cha kufuatilia maboresho ya walimu kitaaluma. Kukosekana kwa mipango sahihi ya mafunzo ya walimu walioko kazini kumesababisha Wizara ya Elimu kukosa chombo ambacho kingeweza kutumika kufuatilia utekelezaji wa mafunzo.

Inajulikana dhahiri kwamba ubora wa elimu unategemea ubora wa vitabu vya kiada vinavyotumika shuleni. Orodha isiyotosheleza ya vitabu vilivyochaguliwa kutumika katika kufundishia na kujifunzia huashiria udhaifu katika ufuatiliaji wa vitabu ambavyo husaidia kufundishia na kujifunzia. Hii pia ilisababisha hali ya kutokuwa na usahihi wa vitabu vya kiada katika soko. Pia, iligundulika kwamba baadhi ya vitabu vya kiada vilivyotumika katika shule havikuwa vimeidhinishwa. Hata hivyo, suala hili halikuzungumziwa na matokeo ya ukaguzi. Masuala mengine yanaohusishwa na udhaifu wa ufuatiliaji ni kama inavyoonekana katika Jedwali 5.1.

**Jedwali 5.1: Masuala ya ukaguzi wa ubora wa elimu yanayohusishwa na udhaifu wa ufuatiliaji**

| Suala | Udhaifu wa ufuatiliaji uliobainishwa |
|---|---|
| Ajira na upangaji wa walimu katika shule mbalimbali sio suala linalochukuliwa kwa umakini/kutiliwa mkazo | Ufuatiliaji usiotosheleza wa upangaji wa shughuli za walimu. |
| Vituo vya kujengea uwezo walimu visivyofanya kazi | Matokezo yanayotarajiwa kutoka katika kituo cha kujengea walimu uwezo hayafikiwi kutokana na ufuatiliaji usiotosheleza. |
| Taarifa za uchunguzi wa Matokeo ya mitihani hazitolewi kwa wakati. | Ufuatiliaji dhaifu wa utendaji wa idara inayohusika na uchunguzi wa matokeo ya mitihani. |

Kadhalika, katika suala la Utoaji wa Huduma za Ugani kwa wakulima, ukaguzi umebaini kukosekana kwa ufanisi unaohusishwa na ufuatiliaji. Tathmini ya ufuatiliaji wa huduma za ugani ulibainisha udhaifu katika suala la kuwepo kwa mipango ya ufuatiliaji iliyoandaliwa na ziara za usimamizi zisizotosha kwa halmashauri.

Ilitarajiwa kwamba Wizara ya Kilimo, Mifugo, na Maendeleo ya Uvuvi; na Ofisi ya Rais - TAMISEMI zingeandaa mipango ya ufuatiliaji kama mwongozo wa kutathminia matokeo na athari za huduma za ugani zinazotokea kutokana na rasilimali za pamoja zinazopitia halmashauri zote. Kufanya ufuatiliaji kwa kuzingatia mipango dhaifu kumesababisha tathmini isiyo ya kutosha ya utendaji wa huduma za ugani za kilimo. Masuala mengine yanayohusishwa na udhaifu katika utoaji wa huduma za ugani ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali 5.3

**Jedwali 5.3: Masuala ya Kiukaguzi wa huduma za ugani yanayohusishwa na udhaifu katika ufuatiliaji.**

| Suala | Udhaifu ulioonekana katika ufuatiliaji |
|---|---|
| Kutowekwa kipaumbele kwa shughuli za ugani katika hatua ya kupanga inapelekea kuondolewa kwa huduma muhimu za ugani katika bajeti. | Ufuatiliaji dhaifu katika upangaji wa shughuli |
| Uhaba wa Maofisa Ugani ni matokeo ya ufuatiliaji hafifu wa huduma za ugani. | Ufuatiliaji dhaifu wa ukuaji wa wakulima dhidi ya huduma za ugani zilizohitajika. |
| Ukosefu wa vitabu vya rejesta vya kilimo katika halmashauri | Ufuatiliaji dhaifu wa ziara za shughuli za usimamizi |
| Ufikiaji wa malengo ya ziara za usimamizi dhaifu na kukosekana kwa mwongozo wa vigezo kwa ajili ya kuchagua maeneo ya kufikiwa kwa kila ziara na lengo la ziara | Mpango kwa ajili ya ziara za usimamizi hazifuatiliwi vizuri. |
| Kukosekana kwa hatua za marekebisho ili kuboresha hali | Kukosekana kwa mfumo sahihi wa kufuatilia utendaji na utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa |

Uchunguzi wa kina kwa ajili ya kubaini uwepo wa wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea na milipuko ya magonjwa haukufanyika kama inavyotakiwa kwa sababu utaratibu wa ufuatiliaji haukuwa wa kutosha kushughulikia uchunguzi kwa ajili ya kubaini uwepo wake. Utekelezaji wa mikakati kwa ajili ya udhibiti wa wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea ulionesha kuwa ufuatiliaji haukufanyika kwa kuangalia ubainishaji wa wadudu waharibifu na magonjwa ya milipuko.

Kwa mfano, kwa miaka kumi iliyopita, uchunguzi wa kina ulifanywa mara moja tu juu ya magonjwa ya mazao. Hii ilishuhudia kutolewa kwa ripoti ya kina juu ya mwitikio kwa ajili ya Usimamizi na Udhibiti wa Ugonjwa wa Mahindi unaoitwa "Lethal Necrosis Disease" katika eneo la Afrika Mashariki mwaka 2013. Utaratibu hafifu wa ufuatiliaji ulipelekea kutoandaliwa kwa mipango iliyozingatia kuwepo kwa usimamizi wa wadudu waharibifu na kutokea kwa milipuko.

Ilibainika kwamba shughuli za ufuatiliaji wa upatikanaji wa mbegu zilizoboreshwa na mbolea kwa ajili ya kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa haukufanyika kwa kiasi cha kutosha. Matokeo yake ruzuku hazikutolewa kikamilifu. Hii ilisababisha wakulima kutumia mbegu za kienyeji zenye uwezo mdogo wa kuzalisha na zinazoshambuliwa na magonjwa makubwa na wadudu waharibifu wa mimea.

Matokeo mengine ya ukaguzi yaliyotokana na udhaifu katika ufuatiliaji ni kama ifuatavyo;

- Upungufu wa utekelezaji wa utabiri wa wadudu waharibifu wa mimea na milipuko ya magonjwa nchini Tanzania.
- Upungufu wa mgawanyo wa rasilimali kwa ajili ya usimamizi wa wadudu waharibifu wa mimea na milipuko ya magonjwa.
- Uratibu dhaifu kati ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na Taasisi za Utafiti wa Viuatilifu nchini.
- Kukosekana kwa mfumo wa kuaminika kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za matukio ya milipuko
- Ukaguzi duni katika vituo vya kupokelea wageni wa kimataifa.

Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Mchakato wa Tathmini ya Athari za Kimazingira katika Miradi ya Maendeleo pia ilionesha kwamba kulikuwa na udhaifu katika ufuatiliaji ambao ulipelekea usimamizi hafifu wa mchakato. Ilibainika kwamba si miradi yote ya maendeleo ilisajiliwa kwa kufuata mchakato wa tathmini ya athari ya kimazingira. Hii ilitokana na ukosefu wa utaratibu wenye lengo la kuleta tija katika kutambua miradi isiyosajiliwa. Kulikuwa na matukio yaliyoripotiwa ambapo vibali vilitolewa bila uthibitisho wa maamuzi ya tathmini ya athari za kimazingira (hali iliyotokana na ufuatiliaji dhaifu wa mchakato.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lilikadiria kiwango cha chini cha idadi ya taarifa zilizopangwa kupitiwa kwa mwaka. Matokeo yake, idadi halisi ya mapitio ya taarifa ilionekana kuwa juu kwa miaka ya ukaguzi. Malengo yaliyowekwa yalionesha mwenendo wa kuongezeka kwa ujumla.

Jedwali 5.4[31] chini linaonesha utofauti kati ya mipango na mafanikio ambapo idadi ya taarifa zilizopitiwa zilikuwa kubwa kuliko idadi zilizolengwa kwa miaka mitano.

**Jedwali 5.4: Lengo na mafanikio ya kupitia taarifa ya tathmini ya athari za mazingira**

| Mwaka | Utofauti (Asilimia) |
|---|---|
| 2010/2011 | 192 |
| 2011/2012 | 108 |
| 2012/2013 | 17 |
| 2013/2014 | 271 |
| 2014/2015 | 40 |

**Chanzo: Mipango ya mwaka ya Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira 2010-2014 na taarifa za mwaka**

[31] Kwa uchambuzi tafadhali rejea Jedwali 4.5

Vilevile, Ukaguzi wa Usimamizi wa Mikataba ya Ujenzi katika Miradi ya Maji Mijini umebaini kwamba udhaifu katika ufuatiliaji ulipelekea usimamizi hafifu katika ujenzi wa miradi ya maji mijini. Ubunifu wa miradi, mapitio, na maandalizi ya nukuu za gharama za ujenzi zilifanywa kwa udhaifu uliotokana na kutokuwepo kwa ufuatiliaji wa kutosha. Hakukuwa na utaratibu wa ufuatiliaji wenye kuleta tija ambao ungeweza kuhakikisha kwamba ubunifu wa zamani unafanyiwa marekebisho kwa kiwango cha kutosha. Utafiti wa kutambua maumbile ya nchi katika eneo la mradi na stadi za miamba haukufanyika kiufanisi kutokana na kukosekana kwa utaratibu wa kufuatilia vipimo. Udhaifu katika ufuatiliaji pia ulipelekea:

- Vibanda vya maji 19 na sehemu ya bomba la kusafirishia katika kipande cha mradi cha kufanyia kazi F & H vijengwe katika miliki ya hifadhi ya barabara ya Wakala wa Taifa wa Barabara;

- Kuongezeka kwa wanufaika wa mradi ambao hawakuwemo mwanzoni kulitokana na ufuatiliaji hafifu wa upembuzi yakinifu uliofanyika;
- Kubadilika kwa bei ya mkataba wakati wa utekelezaji wa mradi kulipelekea kuongezeka kwa gharama;
- Wakandarasi kutozingatia matakwa ya mkataba ya kuajiri wafanyakazi wa msingi wenye sifa zinazohitajika;
- Utumiaji wa vifaa vya ujenzi visivyokuwa na ubora unaotakiwa. Hii ilionekana wakati mkandarasi alipoomba kubadilisha aina ya vifaa vya ujenzi kutumika katika mradi ingawaje kulikuwa na mwongozo maalumu wa aina ya vifaa vitakavyotumika. Bila kufikiria kukataliwa kwa ombi kutoka kwa mhandisi mshauri, bado Wizara iliidhinisha matumizi ya vifaa vya bomba aina ya HDPE ambapo kwa upande mwingine haikufanya kazi kama ilivyotarajiwa.

## 5.4 Tathmini katika utendaji wa sekta ya umma

Tathmini inaweza kuchukuliwa kama jambo linalofanyika mwishoni mwa mradi, ambapo huuangalia iwapo mradi baada ya kukamilika, mradi husika ulifanikiwa au la. Kimsingi tathmini inapaswa kuwa sehemu muhimu ya mradi wowote au uliopangwa tangu mwanzoni. Lengo hasa la tathmini si tu kutafuta nini kilichotokea, bali pia kutumia taarifa kufanya maboresho katika utekelezaji wa mradi au kazi. Tathmini ya taasisi inahitaji kuangalia maeneo katika hatua mbalimbali za kutekeleza shughuli zake wakati ikijiuliza masuala kama inavyooneshwa katika Jedwali 5.5.

**Jedwali 5.5: Masuala yanayoulizwa katika hatua mbalimbali utekelezaji wa kazi**

| *Kutathmini mchakato* |
|---|
| • Endapo tathmini sahihi ilfanyika kujua hitaji halisi na tathmini zilitambua na kuitikia mahitaji.<br>• Endapo mradi uliwekwa na kuendeshwa ndani ya muda uliopangwa na miundo iliyowekwa.<br>• Endapo waliwashirikisha watu waliolengwa.<br>• Endapo wamepata rasilimali zilizotarajiwa.<br>• Endapo wafanyakazi walipewa mafunzo na kuandaliwa kufanya kazi.<br>• Endapo kumbukumbu zilifanywa kiusahihi na kwa wakati. |
| *Kutathmini utekelezaji* |
| • Endapo walifanya kile kilicholengwa<br>• Endapo njia sahihi ilitumika<br>• Endapo hatua ya kazi ililengwa<br>• Endapo kwa kudhamiria au kwa kutokudhamiria mabadiliko yalifanywa, na kwa nini |
| *Matokeo ya Kutathmini* |
| • Endapo kazi iliyofanyika ina matokeo yaliyotarajiwa<br>• Endapo kuna athari nyingine zisizoonekana<br>• Je, athari zilikuwa chanya au hasi (au hakuna kati ya hizi)?<br>• Nini kilihitajika kubadilishwa kama ilihitajika na kwa namna gani ili kuifanya kazi iwe ya tija zaidi. |

Kama inavyoonekana katika Jedwali 5.5, ufuatiliaji wa karibu unahitajika katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa programu. Lengo ni kukusanya taarifa na kisha kuzichambua ili kuhakikisha taarifa zinazopatikana zinaweza kutumika ili kujua endapo taasisi au programu inafanya kazi zilizopangwa kwa ufanisi, na kwa kiwango ambacho itafikia malengo yake na matokeo yaliyotarajiwa.

Hata hivyo, kaguzi za ufanisi zilizofanyika zimebaini udhaifu katika kiwango ambacho taasisi husimamia tathmini zinazopelekea mapungufu ya kiutendaji. Kuwepo kwa walimu wasiokuwa na sifa za kitaaluma katika Ukaguzi wa Mfumo wa Udhibiti wa Ubora wa Elimu ilikuwa ni ishara ya udhaifu katika tathmini ya ndani ya idara zinazohusika kwa kutoa elimu ambayo ingeweza kuwa imebaini uwepo wa walimu wasiokuwa na sifa za kitaaluma.

Mapungufu pia yalionekana katika utekelezaji wa tathmini zilizopangwa. Tathmini ya masuala yaliyoonekana kuhusishwa na tathmini ya udhaifu ni kama inavyoonekana katika Jedwali 5.6.

**Jedwali 5.6: Masuala ya kiukaguzi wa ubora wa elimu yahusianayo na udhaifu katika tathmini**

| Suala | Mapungufu yaliyobainika |
|---|---|
| Kutokuwepo kwa programu za kuendeleza taaluma za walimu | Tathmini hafifu ya programu za kuendeleza taaluma za walimu ambayo hupelekea kufanyika kwa maamuzi ya upangaji wa rasilimali. |
| Vituo vya kujengea uwezo walimu visivyofanya kazi | Tathmini ya kituo cha kujengea walimu uwezo walimu hakijajikita katika kutoa matokeo. |
| Kuchelewa kupandishwa madaraja walimu. | Tathmini ya walimu kupandishwa madaraja haikutoa matokeo yaliyotarajiwa. |
| Wakaguzi hawakuhakikisha vitabu vilivyoidhinishwa vilitumika katika shule | Tathmini ya kazi ya wakaguzi haikulenga kutimiza malengo |
| Kutotekelezwa kwa mapendekezo ya matokeo ya mtihani kuhusiana na maboresho kwenye mtaala. | Tathmini hafifu ya matokeo ya mitihani kuzungumzia masuala ya mtaala. |
| Uratibu duni kati ya TAMISEMI na Sekta za Wizara. | Tathmini hafifu ya Kiwizara ambayo imepelekea pengo kati ya TAMISEMI na Sekta za Wizara. |

Ukaguzi wa Udhibiti Usafi katika Uzalishaji wa Nyama ulibaini tathmini hafifu ya kiidara/kitaasisi ambayo imepelekea idadi ya wanyama waliochinjwa katika machinjio mengi kuzidi uwezo wa machinjio. Masuala mengine yaliyoonekana kuhusiana na tathmini duni ni kama inavyoonekana katika Jedwali 5.7.

**Jedwali 5.7: Masuala ya kiukaguzi wa udhibiti wa usafi katika uzalishaji wa nyama yanayohusiana na tathmini hafifu**

| Suala | Mapungufu yaliyobainika |
|---|---|
| Shughuli za kuchinja zilifanyika pasipo hali ya usafi | Tathmini ya usafi katika machinjio haikufanyika kwa kiasi cha kutosha |
| Udhibiti hafifu wa ubora wa mchakato wa ukaguzi wa nyama | Shughuli za udhibiti ubora zilitathminiwa kimapungufu |
| Taarifa za halmashauri kutoeleza hali ya uchafu katika uzalishaji nyama. | Tathmini iliyofanywa haikuwa ya kina. |

Uwezeshaji usiokuwa wa uhakika wa huduma za ugani unaweza kuwa matokeo ya tathmini kutofanyika vizuri na matokeo yake kulikuwa na kupungua kwa upangaji wa msaada wa kifedha wa kujenga uwezo wa halmashauri. Maeneo ya maonesho na mashamba darasa yalionekana kuwa yameandaliwa kihafifu na kufikishwa katika vijiji. Hali hii inaweza ikawa imesababisha udhaifu katika tathmini ya maeneo ya maonesho na mashamba darasa na kupelekea kushindwa katika kutambua matatizo yanayojitokeza.

Tathmini ya programu za kilimo ili kuonesha masuala ya wadudu waharibifu wa mimea na milipuko ya magonjwa haikufanyika kwa kiwango cha kutosha hivyo kupelekea kuongezeka kwa tatizo la wadudu waharibifu wa mimea na milipuko ya magonjwa nchini Tanzania. Hali hii iliathiri shughuli za uchunguzi wa kina kwa ajili ya utambuzi wake.

Tathmini ya programu za kilimo ili kuelezea masuala ya wadudu waharibifu wa mimea na milipuko wa magonjwa haikufanyika kwa kiwango cha kutosha na kusababisha kuongezeka kwa tatizo la wadudu waharibifu wa mimea na milipuko ya magonjwa Tanzania. Shughuli zinazohusiana na uchunguzi wa kina kwa ajili ya utambuzi wa wadudu waharibifu wa mimea na milipuko ya magonjwa hazikufanyiwa tathmini za mara kwa mara

Iligundulika zaidi kuwa tathmini ya shughuli zinazohusiana na mipango hazikuhakikisha kuwa mipango ya kukabiliana na athari inaandaliwa. Matokeo yake shughuli zilifanyika kwa kushitukiza. Hii iliathiri wakulima kutokana na uzalishaji mdogo hivyo kutokuwepo kwa uhakika wa chakula. Masuala mengine yanayohusiana na udhaifu katika tathmini ni kama vile:

- Mfumo wa kutunza kumbukumbu haukufanyiwa tathmini vya kutosha na matokeo yake ilikuwa vigumu kuchambua magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea. Pia haukuonesha mwenendo/mtiririko katika kanda zote.

- Shughuli za ukaguzi katika sehemu za mipaka ya kimataifa hazikufanyika kwa kiwango cha kutosha.
- Mapungufu katika tathmini ya kiidara ilipelekea uratibu dhaifu kwa shughuli za usimamizi wa wadudu waharibifu wa mimea na magonjwa katika ngazi ya Sekretariati ya Mkoa.

Katika Ukaguzi wa Usimamizi wa Mchakato wa Tathmini ya Athari za Kimazingira katika Miradi ya Maendeleo, mapungufu yafuatayo yanayohusiana na tathmini yalionekana:

- Tathmini ya shughuli za utoaji wa vibali haikufanywa kikamilifu;
- Udhaifu katika tathmini ya Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambao ungeweza kubaini mapungufu yao;
- Tathmini ya shughuli kupitia taarifa ya kuonesha wigo wa kazi ya Tathmini ya Athari za Kimazingira na Hadidu Rejea na utoaji wa taarifa kwa wawekezaji/wenye miradi haukufanyika;
- Tathmini katika uchaguzi wa uundaji wa kamati ya kitaalamu kwa timu za kupitia kazi haikufanyika kikamilifu;

Katika Ukaguzi wa Usimamizi wa Mikataba ya Ujenzi katika Miradi ya Maji Mijini uliofanyika katika Wizara ya Maji, mapungufu yafuatayo katika tathmini yalibainika;

- Tathmini ya kuonesha eneo la miradi haikufanyika;
- Tathmini ya kufuatilia mpango wa kazi haukufanyika kikamilifu;
- Tathmini ya maombi na maidhinisho ya kuongeza muda wa mikataba haikufanyika kwa wakati;
- Tathmini ya kuongeza muda na kuongezeka kwa gharama za kuendesha ofisi hazikufanyika kwa wakati ambapo ingeweza kupunguza kuongezeka kwa gharama za ziada; na
- Tathmini ya gharama anazolipa mkandarasi kwa mwenye mradi kwa kuchelewa kumaliza kazi haikufanywa kwa wakati.

## 5.6 Mawasiliano katika Utendaji wa Sekta ya Umma

Mawasiliano yenye ufanisi ni muhimu kwa taasisi za serikali ili kufanya kazi za msingi za usimamizi kama vile upangaji, kuandaa, kuongoza na kudhibiti. Mawasiliano huwawezesha watawala kufanya kazi na kutimiza wajibu wao. Mawasiliano hutumika kama msingi kwa ajili ya mipango. Taarifa zote za msingi lazima zifanyiwe mawasiliano kwa watawala ambao kwa namna nyingine lazima wafanye mawasiliano ya mipango ili kuitekeleza. Maandalizi pia huhitaji mawasiliano kamili na wengine kuhusu kazi zao. Vilevile, viongozi kama watawala lazima wafanye mawasiliano kikamilifu na wafanyakazi walio chini yao ili kufikia malengo ya pamoja. Udhibiti hauwezekani bila mawasiliano yaliyoandikwa au kwa njia ya mdomo.

Imebainika katika kaguzi nyingi zilizofanyika kwamba taasisi na programu zilikosa mawasiliano kamili ya matokeo ambayo ni muhimu kwa uwajibikaji wa rasilimali walizopewa. Ujirudiaji wa mapungufu katika sekta ya umma kunaweza kusababishwa na tathmini isiyo kamilifu ya mkakati wa mawasiliano. Kwa ujumla, mapungufu yaliyoonekana yalihusu mambo yanayohitajika kufanyiwa mawasiliano na kwa nani; namna gani ya kufanya mawasiliano: wakati gani wa kufanya mawasiliano; na nini kinatarajiwa kutokana na mawasiliano. Jedwali 5.8 linaonesha mapungufu yaliyoonekana sehemu zote katika taasisi zilizokaguliwa.

**Jedwali 5.8: Mapungufu yaliyoonekana katika kila sehemu katika taasisi zilizokaguliwa**

| JINA LA UKAGUZI | TAASISI KAGULIWA | MAPUNGUFU YALIYOONEKANA KILA SEHEMU |
|---|---|---|
| Udhibiti wa Ubora katika Elimu | Wizara ya Elimu, Sayansi, Tekinolojia na Mafunzo ya Ufundi<br>Ofisi ya Rais - TAMISEMI | • Ukosefu wa njia mbalimbali za usambazaji, ikijumuisha taarifa zilizoandikwa, vyombo vya elektroniki na mawasiliano ya ana kwa ana<br>• Kutokuundwa kwa mifumo iliyo wazi ili watumiaji kufanya mahitaji yao na vipaumbele vyao kutambulika na taasisi.<br>• Kutokuwepo kwa utaratibu wa kudhibiti ubora wa kuhakikisha kwamba taarifa ni sahihi, inayohusika na inayowakilisha |

| JINA LA UKAGUZI | TAASISI KAGULIWA | MAPUNGUFU YALIYOONEKANA KILA SEHEMU |
|---|---|---|
| Udhibiti wa Usafi katika Uzalishaji wa Nyama. | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | • Ukosefu wa njia mbalimbali za usambazaji, ikijumuisha taarifa zilizoandikwa, vyombo vya elektroniki na mawasiliano ya ana kwa ana<br>• Kutokuundwa kwa mifumo iliyo wazi iliwatumiaji waweze kutimiza mahitaji yao na vipaumbele vyao kutambulika na taasisi.<br>• Kutokuwepo kwa utaratibu wa kudhibiti ubora, na kuhakikisha kwamba taarifa ni sahihi,inayohusika na inayowakilisha |
| Huduma za Ugani | Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi | • Ukosefu wa njia mbalimbali za usambazaji, ikijumuisha taarifa zilizoandikwa, vyombo vya elektroniki na mawasiliano ya ana kwa ana<br>• Kutokuundwa kwa mifumo iliyo wazi kwa watumiaji kili waweze kutimiza mahitaji yao na vipaumbele vyao kutambulika na taasisi.<br>• Kutokuwepo kwa utaratibu wa kudhibiti ubora na kuhakikisha kwamba taarifa ni sahihi,inayohusika na inayowakilisha |
| Tathmini ya Athari za Kimazingira | Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira | • Ukosefu wa kushirikishana taarifa kutoka Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwenda halmashauri kwa kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI<br>• Ukosefu wa mawasiliano kwa wadau husika ambao hawajakidhi matakwa ya Tathmini ya athari ya Kimazingira au Ukaguzi wa Mazingira<br>• Mawasiliano ya matokeo ya uchunguzi kwa wawekezaji/wenye miradi ndani ya muda uliotakiwa |
| Milipuko ya Magonjwa na Wadudu Waharibifu wa Mimea | TAMISEMI | • Mtiririko dhaifuwa mawasiliano kwenye milipuko wa magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea<br>• Utoaji wa mafunzo wenye masuala yasiyotosha kuhusu mlipuko wa magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea |
| Usimamizi wa Mikataba Katika Ujenzi wa Miradi ya maji | Wizara ya Maji na Umwagiliaji | • Mfumo wa mawasiliano usiofaa na usiotumia maandishi kutoka Wizara ya Maji kwenda kwa Mkandarasi<br>• Kutokuwepo kwa utaratibu wa kudhibiti ubora wa kuhakikisha kwamba taarifa ni sahihi,inayohusika na inayowakilisha |

**Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi**

Jedwali 5.8 hapo juu linaonesha muhtasari wa mapungufu yaliyojitokeza katika kila sehemu yanayohusiana na mawasiliano kama yalivyoonekana katika kaguzi zilizofanywa katika taasisi husika za serikali. Mapungufu hayo yanaelezewa kimahususi hapa chini.

Ukaguzi wa Mfumo wa Udhibiti wa Programu za Ubora wa Elimu ulibaini matokeo ya ukaguzi uliotokana na udhaifu katika mawasiliano. Matokeo ya mitihani hulenga katika kuwapa wadau taarifa zinazotakiwa kwa maboresho. Hata hivyo, ilionekana kwamba matokeo ya mitihani hayakutumika kwa ajili ya maboresho ya taasisi zilizohusika katika kutoa elimu. Kulikuwa na utolewaji wa ripoti za uchunguzi wa matokeo ya mitihani usiyozingatia muda na usambazaji duni wa ripoti za uchunguzi. Hivyo, taasisi zinazohusika katika kutoa elimu nchini hazikutumia taarifa kikamilifu kuandaa mipango kwa kuzingatia utendaji wa taasisi.

Mawasiliano yasiyofaa au mawasiliano yaliyocheleweshwa yanaweza kupelekea utekelezaji usiokamilika wa mapendekezo yaliyotolewa. Hii inashuhudiwa katika ripoti ya ukaguzi kuhusu udhibiti wa usafi katika uzalishaji nyama ambao uliripotiwa kuwepo kwa utekelezaji duni wa mapendekezo yaliyotolewa. Moja ya mapendekezo yalionesha kasoro ndogo katika utendaji na za mazingira kama vile kuondoa sakafu iliyoharibika, kuboresha mfumo wa usimamizi wa taka, kuhakikisha kuwepo kwa maji ya kutosha, na utupaji sahihi wa taka.

Mapendekezo mengine yalitaka kufungwa kwa machinjio (majengo). Pia kulikuwa na maboresho makubwa yaliyokuwa yakisubiria kuhakikishwa. Miongoni mwao ni kuhakikisha kwamba uchinjaji unafanyika katika maeneo sahihi, uuaji wa vijidudu katika vifaa vya uchinjaji, utupaji sahihi wa taka zilizozalishwa, na ukaguzi wa wanyama kabla ya kuchinja. Hata hivyo, ilibainika kwamba asilimia 25 tu ya mapendekezo yaliyotolewa yalitekelezwa kikamilifu.

Kutokujua umuhimu wa kitu cha kuwasiliana huweza kupelekea kuacha masuala muhimu kama vile kushirikishana ripoti kwa wadau wanaohusika. Hali hii imebainika katika ukaguzi wa udhibiti wa usafi katika uzalishaji wa nyama ambapo hakukuwa na kushirikiana katika ripoti za ufuatiliaji miongoni mwa wizara zilizohusika kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba nyama salama inatolewa kwa umma.

Vilevile, katika ukaguzi wa utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima, kutokuwepo kwa kitabu cha rejesta ya kilimo katika halmashauri kulizuia kukamilika kwa uwekaji kumbukumbu za shughuli za ugani za kila siku. Taarifa zilizokuwepo ndani ya vitabu vya rejesta zingeweza kuwafahamisha wafadhili juu ya masuala kama vile idadi ya wakulima waliopo, aina ya mazao yaliyolimwa, na ratiba ya kufanya kazi ya maofisa ugani ambayo huonesha shughuli/kazi zifanywazo na kata na/au maofisa ugani wa kijiji kwa kila siku.

Usimamizi wa sheria unahitaji mawasiliano ya kutosha kwa wadau husika. Hata hivyo, udhaifu katika mawasiliano haukuwezesha taarifa kuwafikia kwa wakati kundi lililolengwa. Hivyo, wadau hawajui masharti yanayotakiwa kwa ajili ya kuendesha machinjio. Pia, miongozo ya huduma za ugani ambayo ilitakiwa kugawiwa kwa halmashauri zote haikugawiwa. Hii imesababisha fedha zilizopangwa kwa ajili ya huduma za ugani zitumike kwa shughuli nyingine.

Mfumo wa utoaji taarifa usio wa ufanisi ulisababisha uhaba wa miongozo ya huduma za ugani katika halmashauri; kutohamasishwa umuhimu wa miongozo ya huduma za ugani; na fedha kwa ajili ya huduma za ugani kutumika kwa ajili ya shughuli nyingine. Taarifa kuhusu milipuko ya magonjwa hazikufikishwa kwa wakati. Matokeo yake, idadi ya mikoa iliyoathirika iliongezeka. Kutokufanya mawasiliano kuhusu miongozo ya upangaji imepelekea kutokuandaliwa vizuri kwa mipango ya kukabiliana na athari. Hii husababisha halmashauri kushindwa kudhibiti na kusimamia milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea. Ilibainika pia kwamba matokeo ya utabiri hayakupelekwa katika idara husika. Matokeo yake mtego wa kutabiri kuwepo kwa wadudu waharibifu wa mimea unaoitwa Pheromone haukutunzwa.

Vilevile, wakulima na maofisa ugani hawakufahamishwa vizuri kuhusu elimu inayohusiana na uchunguzi wa kina. Mfumo duni wa mawasiliano ulipelekea taarifa za milipuko ya magonjwa kupokelewa kwa nadra kutoka Sekretariati za Mikoa na kusababisha uratibu hafifu wa usimamizi wa shughuli za wadudu waharibifu wa mimea na magonjwa katika Mikoa.

Muhtasari wa masuala yaliyochukuliwa kutoka kwenye matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na mawasiliano ni kama inavyoonekana katika Jedwali 5.9.

**Jedwali 5.9: Chati inayoonesha Ufuatiliaji wa Mawasiliano**


| Ukaguzi | Watu waliolengwa | Malengo ya mawasiliano | Zana ya mawasiliano | Hali iliyopo |
|---|---|---|---|---|
| Mfumo wa Usimamizi wa Ubora wa Elimu | Shule | Kuwa na walimu wenye sifa | Taarifa za Mwaka | Walimu wasiokuwa na ujuzi waliopo |
| | Walimu | Mafunzo kazini | Mipango ya mafunzo | Mafunzo duni |
| | Walimu | Kupandishwa madaraja kwa wakati | Tathmini ya walimu | Upandishaji madara kuchelewa |
| | Wazazi/wanafunzi/walimu | Vitabu sahihi | Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa | Isiyo ya kina |
| | Umma | Tathmini ya wanafunzi | Ripoti ya mitihani | Kutofikiwa wadau wote |
| Udhibiti wa Usafi katika Nyama | Umma | Nyama salama | Usafi wa machinjio | Mazoea ya hali ya uchafu katika machinjio |
| Huduma za Ugani | Wakulima | Kuboresha teknolojia ya kilimo kwa wakulima | Kutwaa teknolojia ya kilimo | Uzalishaji mdogo |
| Tathmini ya Athari za Mazingira | Mwanajumuiya /umma | Kupokea taarifa kwa wakati | Vyombo vya habari | Kuchelewa kupokelewa kwa taarifa |

| Ukaguzi | Watu waliolengwa | Malengo ya mawasiliano | Zana ya mawasiliano | Hali iliyopo |
|---|---|---|---|---|
| Wadudu Waharibifu wa Mimea | Wakulima | Kuboresha ujuzi katika udhibiti wa wadudu waharibifu wa mime na magonjwa | Mpango wa mafunzo | Mafunzo duni |
| Usimamizi wa Mikataba | Makandarasi | Kupokea taarifa kwa wakati | Maelekezo kutoka kwa mshauri | Kuchelewa kupokelewa kwa taarifa |

Jedwali 5.9 linaonesha kwamba taasisi zilizokaguliwa zilikuwa zimetambua kile kilichohitajika kwa ajili ya kukifanyia mawasiliano, kwa mlengwa na kwa namna gani. Hata hivyo, bado kuna tatizo, ambapo lengo la jumla la mawasiliano kwa kuzingatia malengo ya kitaasisi bado hayajafikiwa.

Ufuatao ni uhusiano wa matokeo ya ukaguzi na ufuatiliaji kama ilivyowekwa kwa ufupisho katika Kielelezo 5.1 hapo chini:

**Kielelezo 5.1: Uhusiano wa Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Ufuatiliaji Katika Sekta ya Umma**



# SURA YA SITA

# HITIMISHO

## 6.0 Utangulizi

Uchambuzi wa masuala yaliyobainika katika kaguzi sita za ufanisi zilizofanyika unaifanya Ofisi ya Ukaguzi wa Hesabu kuhitimisha kwamba kuna mapungufu ya utendaji yanayohusiana na usimamizi wa data, upimaji wa utendaji, na ufuatiliaji katika utendaji wa sekta ya umma. Hivyo, mafanikio ya baadhi ya malengo ya serikali yaliyopangwa yanaweza kuonekana kutokana na idadi ya mapungufu yaliyobainishwa katika kaguzi. Hitimisho maalumu ni kama ilivyo hapa chini.

## 6.1 Usimamizi wa data kwenye shughuli za sekta za umma

Taasisi za serikali haziweki kumbukumbu za taarifa mbalimbali ipasavyo kwa sababu ya mapungufu katika matumizi ya mifumo ya kurekodi taarifa kutoka vyanzo mbalimbali. Zaidi, kuna mapungufu katika kupitia taarifa zinazopokelewa na taasisi husika kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani na vya nje kwa sababu ya kutokuwa na mfumo madhubuti wa kunakili taarifa. Matokeo yake taasisi hizo zimeshindwa kutoa au kuzalisha taarifa ambazo zinaashiria hali halisi ya shughuli za serikali.

Kwa upande mwingine, taasisi za serikali hazizalishi taarifa sahihi wakati wa kutekeleza shughuli zake na matokeo ya matumizi ya taarifa hizo hayanakiliwi au kuwekwa kwenye kumbukumbu ipasavyo na kwa wakati. Kulikuwa pia na mapungufu kwenye usahihi wa mifumo ya kuingiza taarifa ndani ya taasisi husika. Hakukuwa na vitengo vya kuchukua na kuzalisha taarifa ambavyo vingekuwa sehemu ya kupatia kumbukumbu na pale ambapo vitengo hivyo vilikuwepo vilibainika kuwa na mapungufu.

Kwa upande mwingine, taasisi za serikali hazizalishi taarifa sahihi wakati wa kutekeleza shughuli zake na matokeo ya matumizi ya taarifa hizo hayanakiliwi au kuwekwa kwenye kumbukumbu ipasavyo na kwa wakati. Kulikuwa pia na mapungufu kwenye usahihi wa mifumo ya kuingiza taarifa ndani ya taasisi husika. Hakukuwa na vitengo vya kuchukua na kuzalisha taarifa ambavyo vingekuwa sehemu ya kupatia kumbukumbu na pale ambapo vitengo hivyo vilikuwepo vilibainika kuwa na mapungufu.

Taasisi za serikali zimeshindwa kuainisha majukumu ndani ya taasisi kuhusu kuchukua, kuzalisha na kuhakiki taarifa. Hakuna mfumo wa wazi ambao unawezesha taasisi kuhakiki taarifa inazozalisha ndani ya taasisi au zile zinazotoka nje ya taasisi kwa matumizi ya taasisi au ya umma. Hii imeathiri uwepo wa tija wakati wa mchakato wa kupitia taarifa ndani ya taasisi ili kuhakikisha taarifa zote zinahakikiwa na kuwa tayari kwa matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya maamuzi au kuchapishwa.

Mifumo ya uhifadhi wa taarifa haijitoshelezi. Matokeo yake ni kuwa taarifa haziko tayari pale zinapohitajika kwa malengo fulani. Hapakuwa na rejesta za kuhifadhia taarifa zinazopokelewa na zinazozalishwa kutoka ndani au nje ya taasisi. Taasisi za serikali zimeshindwa kuhifadhi kumbukumbu za shughuli zinazofanywa na taasisi husika. Kumbukumbu za ukaguzi, ufuatiliaji, na uthamini au mapitio hazijahifadhiwa kikamilifu katika taasisi husika. Matokeo yake, uwepo na upatikanaji wake haufahamiki. Taarifa zilizokuwepo ndani ya taasisi hazijitoshelezi kuwezesha taasisi au mtumiaji wa taarifa hizo kufanya maamuzi sahihi na ya busara.

Taasisi za serikali hazina sera zinazohusiana na ubora wa taarifa ili kuhakikisha ubora wa taarifa zinazotengenezwa na kuzalishwa na taasisi husika. Taarifa zinazohifadhiwa na taasisi hazitoi mwelekeo wa hali halisi ya taasisi. Kuna tofauti kubwa katika kuelezea suala la aina moja pale linapotolewa taarifa na taasisi tofauti.

Taarifa zinazoandaliwa na taasisi za serikali ni pamoja na takwimu mbalimbali. Hata hivyo taasisi za serikali hazitumi taarifa hizo kwenye taasisi zingine za kisekta kama inavyotakiwa na baadhi ya miongozo ya kiutendaji. Hii imeathiri shughuli za uratibu kwa sababu ya ukosefu wa taarifa kwenye sekta zingine.

Kuna upungufu katika matumizi ya taarifa zilizopo ndani ya taasisi kwa ajili ya kuandaa mipango mbalimbali ya mwaka kwa miaka inayofuata. Matokeo yake, mazoea ya utendaji kwa dharura ndani ya taasisi za serikali imekuwa ikishika hatamu.

Kumekuwa na upungufu katika matumizi ya taarifa katika utoaji wa mrejesho kwenye taasisi zingine za kisekta. Mara taarifa zinapowasilishwa kwenye mamlaka husika, taasisi hizo hazitoi mrejesho wa kutosha kuhusiana na taarifa zilizowasilishwa. Hii imezinyima taasisi zinazowasilisha taarifa fursa ya kuboresha utendaji kwa kutumia mrejesho unaopata kutoka mamlaka husika.

## 6.2 Upimaji wa Utendaji kwa Taasisi za Serikali

### 6.2.1 Kushindwa kusimamia upimaji wa utendaji kwenye taasisi za serikali

Upimaji wa utendaji kwenye taasisi za serikali haufanyiki ipasavyo na kupelekea udhaifu kwenye kupima na kuelewa kiwango cha ufanisi kwenye taasisi mbalimbali za serikali. Hii ni kwa sababu taasisi nyingi za serikali hazijaandaa mifumo ya kupima utendaji ambayo ingewezesha kutoa mwongozo na kuelekeza namna taasisi za serikali zitakavyochanganua utendaji wake katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Sababu nyingine ni kuwa licha ya kuwa taasisi za serikali zinapanga shughuli za kutekelezwa, shughuli hizo zinakosa viashiria husika ambavyo vingeweza kutumika kama mizani ya ulinganifu kwa kutathmini ufikiwaji wa malengo na madhumuni yaliyowekwa kwa huduma zinazotolewa.

Vilevile, upimaji wa utendaji wa taasisi za serikali ni changamoto kwa sababu ya kukosekana kwa mfumo wa kukusanyia data, na kukosekana kwa tathmini na tafsiri ya taarifa za kiutendaji ambazo zinahitajika ili kupima kiwango cha ufanisi kwa shughuli husika. Kwa kiasi kikubwa hali hii imechangiwa na sababu kuu mbili. Sababu ya kwanza ni kushindwa kubainisha aina ya taarifa inayohitajika. Hii inatokana na kukosekana kwa viashiria muhimu vya kupima ufanisi. Sababu ya pili ni udhaifu katika utunzaji wa taarifa muhimu za kiutendaji.

Changamoto nyingine katika taasisi za umma ni katika eneo la utoaji wa taarifa za kiutendaji na mrejesho. Taarifa za kiutendaji zimekuwa zikiripotiwa kwa asilimia ndogo tu. Pia, ni mara chache taasisi zilizopokea au kutuma ripoti zimekuwa zikitoa mrejesho. Hii imekwamisha mchakato mzima wa kupima utendaji katika taasisi za umma. Hivyo taasisi zimeshindwa kufikia madhumuni na malengo yaliyowekwa katika kuhakikisha kunakuwa na uboreshaji kwenye utoaji wa huduma kwa wananchi.

Hivyo basi, wananchi wamekuwa wakipata huduma dhaifu kutoka kwenye taasisi za serikali. Hii inatokana na kuwepo na mapungufu ya kiutendaji kwenye utoaji wa huduma unaofanywa na taasisi za serikali. Hali hii inapelekea taasisi za serikali kushindwa kuchukua hatua za uwajibikaji katika maeneo yanayohitaji uboreshaji zaidi.

## 6.3 Ufuatiliaji katika shughuli za sekta ya umma

Uzito mdogo umepewa kwa ufuatiliaji kwenye utoaji wa huduma za serikali hali inayopelekea mapungufu na utendaji usio wa ufanisi. Kwa kuzingatia matokeo ya ripoti za ukaguzi wa ufanisi, kuna mapungufu yaliyoonekana katika ufuatiliaji, tathmini, na mawasiliano ya matokeo yaliyotarajiwa ya utendaji.

Hii inamaanisha mapungufu katika ufuatiliaji, tathmini, na mawasiliano ya matokeo kwa watumiaji walengwa na hivyo kusababisha udhaifu katika usimamizi katika shughuli za sekta ya umma. Mapungufu katika ufuatiliaji, tathmini na mawasiliano huathiri utendaji mzima wa shughuli na utoaji wa huduma kwa umma.

Pia, wadau wanatekeleza majukumu yao bila ufanisi kwa kuwa hawapewi taarifa kwa wakati. Uratibu mzuri miongoni mwa wadau ulihitaji mawasiliano sahihi na kwa wakati katika hatua ya mwanzo na kushirikishwa kipindi chote cha utekelezaji hadi mwisho wa mradi.

Kuwa na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini pekee katika taasisi za umma hakuhakikishi mafanikio ya matokeo yaliyotarajiwa. Maendeleo katika kufikia matokeo yanahitaji kufuatiliwa, kutathminiwa, na mawasiliano kwa wadau wote wanaohusika. Kadhalika, hakuna kiwango kizuri cha ufuatiliaji, tathmini, na mawasiliano pekee kitakachosahihisha ubunifu wa shughuli, mipango na matokeo.

Mawasiliano kutokana na ufuatiliaji yanahitajika ili kuleta matumaini ya maboresho au kuimarisha mipango. Taarifa kutokana na ufuatiliaji wenye utaratibu pia hutoa mchango muhimu sana kwa tathmini. Ni ngumu sana kutathmini shughuli ambayo haijafanyiwa ubunifu vizuri na ambayo haina utaratibu wa ufuatiliaji wa maendeleo yake na kutoa taarifa kwa matokeo yake.

Tathmini hujazia ufuatiliaji kwa kutoa tathmini ya kipekee na ya kina ya kile kilichotoa matokeo mazuri na kile ambacho hakikutoa matokeo mazuri, na kwa nini imekuwa hivyo. Baada ya kutekeleza na kufuatilia jitihada kwa kipindi fulani, ni muhimu kwa utawala kuchukua hatua ya kufanya tathmini ya hali nje ya mambo.

Tathmini ya ubora hutoa mrejesho ambao huweza kutumika kwa maboresho. Tathmini pia hutambua matokeo yasiyolengwa na matokeo/athari za mipango ya maendeleo, ambayo huenda isiwe katika ufuatiliaji wa mara kwa mara. Hii ni kuwa mipango ya maendeleo hulenga utekelezaji wa mpango wa maendeleo. Taarifa zilizotokana na tathmini huchangia hali ya kujifunza kitaasisi.

Ufuatiliaji, tathmini na matokeo duni waliyowasilishwa huzuia uwepo wa taarifa sahihi ambayo ingeweza kutumika kwa maboresho ya wakati ujao.

# SURA YA SABA

# MAPENDEKEZO

## 7.1 Utangulizi

Sehemu hii inatoa mapendekezo kulingana na hitimisho la hapo juu katika usimamizi wa data, upimaji wa utendaji, na ufuatiliaji katika sekta ya umma.

## 7.2 Usimamizi wa data kwenye shughuli za sekta ya umma

Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kuwa wizara, idara zinazojitegemea, mashirika na mamlaka za serikali za mitaa zinafanya yafuatayo:

(a) Kuanzisha mfumo wa wazi wa kupata, kuandaa, na kuzalisha data ambazo zinafaa kwa taasisi husika ili kuziwezesha kuchukua maamuzi sahihi. Kwa kuzingati hili taasisi za serikali zihakikishe:

   i. Zina kumbukumbu za taarifa zote izipatazo au zinazozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali kwa matumizi ya ofisi na kiutendaji kwa ajili ya shughuli husika.

   ii Zianzishe na kuboresha mifumo ya kitaasisi ambayo itahakikisha kuwa taarifa zote zinazopatikana na kuzalishwa ni sahihi na halisi.

   iii Zianzishe mfumo wa kupitia taarifa zote ili kuhakikisha taarifa zinazopatikana kutoka vyanzo mbalimbali zinafanyiwa mapitio, zimekamilika na sahihi kabla hazijatumika.

(b) Kuanzisha mfumo imara kwa ajili ya utunzaji wa kumbukumbu za taarifa ili kufanikisha uwepo na upatikanaji wa taarifa hizo mara zinapohitajiwa na watumiaji.

(c) Kuandaa sera na mikakati ya usimamizi wa taarifa ndani ya taasisi ili kuimarisha ubora wa taarifa kwenye sekta ya umma.

(d) Kuanzisha mfumo imara wa kuwasilisha na kushirikishana taarifa baina ya taasisi za umma pindi zinapotakiwa kufanya hivyo na miongozo mbalimbali.

(e) Kutoa mrejesho kwa taarifa zinazowasilishwa kwenye taasisi za umma kwa ajili ya kuchukua hatua za marekebisho au maboresho ili kusaidia katika kufanya maamuzi.

**Upimaji wa kiutendaji kwenye taasisi za umma**

Ofisi ya Waziri Mkuu inapaswa kuhakikisha kuwa Wizara, Idara, Taasisi, na Serikali za Mitaa zote:

(a) Zinaanzisha na kuwa na mfumo wa kupima utendaji. Kupitia mfumo huo taarifa za kiutendaji za mwaka za kila taasisi zinaandaliwa na zinatumika kama kipimo cha kutathmini kiwango cha ufanisi kwa huduma zitolewazo;

(b) Zinatayarisha mfumo wa kupima utendaji ambao utajumuisha huduma zote zinazotolewa na taasisi husika, na kutoa hali ya utekelezaji wa utoaji wa huduma hizo kwa kufanya tathmini za mara kwa mara;

(c) Ziwe na mfumo sahihi wa kuainisha na kuchagua viashiria muhimu vya kupima ufanisi ambavyo vitatumika kupima uwajibikaji katika huduma zinazotolewa kwa wananchi;

(d) Ziwe na mfumo madhubuti wa kupatia taarifa, kufanya tathmini, kutafsiri na kuripoti taarifa za kiutendaji kwa taasisi husika; na

(e) Zitekeleze kwa wakati mapendekezo yaliyotolewa na kutoa mrejesho kwa taasisi husika.

## 7.4 Usimamizi wa ufuatiliaji katika sekta ya umma

Ofisi ya Waziri Mkuu inapaswa kuhakikisha kwamba Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika na Mamlaka za Serikali za Mitaa:

(a) Zinabuni mfumo wa ufuatiliaji ili kukusanya takwimu, kuchambua, na kutumia kwa ajili kuongoza ujifunzaji wa mikakati ya ufumbuzi;

(b) Zibuni mfumo wa ufuatiliaji ili kuongoza mtiririko wenye ufanisi wa taarifa kupitia taasisi kwenda kwenye ngazi tofauti za utawala ili kusaidia utoaji wa maamuzi;

(c) Zipitie mara kwa mara na kurekebisha zana zinazotumika kusimamia eneo la tathmini ili kutoa mwelekeo sahihi wa maendeleo ya kiidara ambayo yanaweza kufikiriwa katika mchakato wa tathmini ya usimamizi wa mfumo wa uwajibikaji;

(d) Zitoe mwongozo wa wazi kufuatilia utendaji wa idara katika matumizi ya rasilimali ili tathmini yaliyofanyika na kutoa picha halisi ya kile kinachotokea;

(e) Ziandae taarifa za moja kwa moja zilizotokana na mchakato wa tathmini kwa watumiaji sahihi ili kuwezesha kuchukuliwa hatua zinazohitajika.

(f) Zibaini mara kwa mara mapungufu ya mawasiliano ili kuhakikisha kwamba taarifa zinawasilishwa kwa walengwa kwa ajili ya kuchukua hatua za kiutawala.

## MAREJEO


*i.* Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima nchini Tanzania, *Utendaji wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,* Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Machi ,2015.

ii Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa mikataba ya ujenzi wa miradi ya maji mijini katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji, *Utendaji wa Wizara ya Maji na umwagiliaji,*Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Machi 2016.

iii Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa usafi (Udhibiti uchafu) katika mchakato wa uzalishaji nyama, *Utendaji wa Wizara ya Kilimo,Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi, Ofisi ya Raisi- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Afya,Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wazee na Watoto*,Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Machi 2016.

iv Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Mikakati ya kukabiliana na Milipuko ya Magonjwa na Wadudu waharibifu wa mimea nchini Tanzania, *Utendaji wa Wizara ya Kilimo,Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na Ofisi ya Raisi- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,* Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Machi 2016.

v Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mchakato wa tathmini ya athari za Mazingira katika Miradi ya Maendeleo ,*Utendaji wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira na Ofisi ya Makamu wa Raisi-Idara ya Mazingira,* Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Machi 2016.

vi Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Mfumo wa Usimamizi/Udhibiti Ubora wa Elimu nchini Tanzania ,*Utendaji wa Wizara ya Elimu,Sayansi,Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi na Ofisi ya Raisi- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,* Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Machi 2016.